





**Askari** polisi sita mbaroni tuhuma mauaji kwa risasi

UKURASA 5


Ukurasa 12
Uchaguzi mbunge Mbarali huo, NEC yapuliza kipenga

Ukurasa 13
Kuingia kwenye siasa haikuwa rahisi ilinipasa kubwaga kazi yangu serikalini

Ukurasa 14
Ndivyo kifo cha vigogo wa Wagner kitavyowarudi Putin, Lukashenko

siasa
JUMATANO AGOSTI 30, 2023 Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

KUPANUKA BRICS
Ni kusaidiana wenye vikwazo kupumua, kuinua biashara
• Bado kitendawili namna ambavyo Afrika inavyoweza kunufaika

Na Nimi Mweta

NCHI zinazoendelea na chache zilizoendelea zinazofungamana katika kundi la BRICS zikihusisha mataifa ya Brazil, Russia, India, China, South Africa, zinapanua wigo na kuongeza wanachama wengine.

Viongozi wake wamekutana Afrika Kusini wiki iliyopita ikiwa ni kama mkutano pacha na ule G20 kundi la nchi 20 zilizoendelea kiuchumi duniani unaofanyika Septemba 9 na 10 nchini India.

Wanachama wa kudumu wa kundi la BRICS waliokuwa watano sasa wameongezeka na kufikia 11 na bado wapo waalikwa au watazamaji.

Rais Samia Suluhu Hassan, mathalani, amehudhuria mkutano huo licha ya kuwa Tanzania siyo taifa 'mfikiriwa' wa uanachama BRICS, lakini hakuna tatizo endapo inahitaji kushiriki mikutano katika ngazi tofauti.

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Agosti 30, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581418

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




SAKATA LA BANDARI

# Bunge latoa msimamo

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa nne kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya CRDB Bank Foundation, Martin Warioba (wa tatu kushoto), wakizindua ujenzi wa soko la kisasa la CRDB Kizimkazi Dimbani, Mkoa wa Kusini Unguja jana, linalojengwa kwa ufadhili wa benki hiyo kwa gharama ya Sh. bilioni mbili. **HABARI UK. 4. PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 19

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

**SHAHIDI: TULIKAGUA NYUMBA YA MKE WA MSUYA HADI USIKU WA MANANE**



MKUU wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, SSP David Mwanahe (56), amedai mahakamani kuwa walifanya upekuzi katika nyumba ya aliyekuwa mke wa Erasto...

## Rais aahidi neema sekta binafsi akizindua miradi

UKURASA 3

# Kikokotoo mafao chaibua hoja bungeni

UK.4

**MICHEZO** PHIRI AVUNJA UKIMYA SAKATA NA ROBERTINHO UK.24

**KATUNI** UK.6

SAKATA LA BANDARI

# Bunge latoa msimamo

**Na Romana Mallya,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ametoa msimamo kuhusu sakata la uendelezaji wa Bandari kuwa, kwa sasa Bunge halitatoa ufafanuzi ama kujibu hoja za Watanzania.

Pia amewatoa wasiwasi wananchi kuhusu suala hilo kuwa watalifanyia kazi kama walivyowatuma kuwasimamia bungeni.

Dk. Tulia alitoa kauli hiyo jana akisisitiza kuwa kazi ya Bunge ni kupokea maoni yanayotolewa na wananchi na wakati utakapofika watayatumia kuendelea kuishauri serikali.

"Hatutatumia Bunge hili kutoa ufafanuzi ama kujibu hoja za wananchi, ni kazi yetu kuzipokea hoja hizo, ni kazi yetu kupokea maoni yao na pale tunapoona upo ulazima, basi Bunge litaleta hoja hizo hapa mezani na tutaweza kuzijadili kwa pamoja namna ya kufanya uamuzi kama Bunge," alisema.

Alisema walikwenda majimboni na wamewasikia wananchi wakiwamo ambao siyo wa kutoka majimboni mwao, wakiendelea kutoa maoni kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea nchini.

"Kwa sababu sisi kama wabunge ni wawakilishi wa wananchi, tunawasikiliza wananchi mawazo yao, tunayachakata na kuishauri serikali na yale ambayo tunapaswa kusimamia serikali basi tunaisimamia serikali.

"Kwa kuwa mawazo hayo yametolewa katika maeneo mapana sana kwa maana yamezungumziwa mambo mengi na mengine ni mambo mahususi, yote ni kazi yetu kuyachukua kuyafanyia kazi, kuishauri serikali na yale ambayo tunapaswa kuisimamia serikali, kuendelea kuisimamia," alisema.

Akifafanua, alisema ili wasiwe wanakwenda mbele na kurudi nyuma, kwa jambo mahususi linalohusu uwekezaji bandarini, mawazo yameendelea kutolewa na wananchi baada ya Bunge kufanya uamuzi mwezi Juni.

"Katika upana wa mawanda wa mawazo yaliyotolewa, Bunge hili tulishamaliza kwa sehemu kazi yetu. Kazi itakayofuata baada ya hapo ni ya kuisimamia serikali kwenye jambo ambalo Bunge lilishafanya uamuzi.

"Kwa kuwa Bunge lilishafanya uamuzi, tusije tukajikuta Bunge letu hili tunarejea tena kwenye kutoa mawazo juu ya jambo hili ambalo tulishafanya uamuzi.

Alisema wakati wao wa kuzungumza tena kuhusu suala hilo, itakuwa ni pale ambapo sheria inawapa nafasi nyingine.

"Waheshimiwa wabunge, tukitaka serikali ilete mikataba hapa bungeni kuijadili hoja itakuwa mbele yetu na kwa hivyo, mawazo tunayoendelea kusikia kutoka kwa wananchi wakati huo, tutaweza kuyasema na kuiambia serikali nini inapaswa kufanya kwa sababu tutafanya tena uamuzi mwingine yatakayokuwa yanahusu hoja iliyopo mezani," alisema.

"Ninasema hivi, tusije tukajikuta na sisi tunakuja humu bungeni kutaka kufikiri tunaweza kutumia nafasi hii pengine kutoa ufafanuzi wa yale waliyoyasema ama wakati mwingine kutoa majibu juu ya hoja walizozitoa.

"Wananchi wasiwe na wasiwasi juu ya jambo hili, tutakapotaka kujua mikataba inayoingiwa na serikali inasema nini, sheria zetu tulizozitunga inaturuhusu tutaita mikataba hiyo na wananchi tutawafanyia kazi ile ambayo wametutuma kufanya hapa bungeni ya kuisimamia serikali," alisema Spika Tulia.

Alisisitiza kuwa hawatatumia Bunge hilo kutoa ufafanuzi ama kujibu hoja za wananchi kwa kuwa kazi yao ni kupokea maoni yao na pale wanapoona upo ulazima Bunge litaleta hoja hizo mezani na kuzijadili kwa pamoja na kufanya uamuzi kama Bunge.

**MISWADA 5 UKIWAMO UMILIKI MALI NA MALIASILI YAPITISHWA**

Bunge limepitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (No.2) 2023 unaolenga kurekebisha sheria tano, ikiwamo kuhusu Umiliki wa Mali na Rasilimali Asilia Sura 449 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu masharti hasi katika mikataba ya Mali na Rasilimali Asilia, Sura ya 450.

Marekebisho hayo ni kuhakikisha utekelezaji wa sheria hizo hauathiri utendaji wa maeneo ya bandari, bandari za nchi kavu na bandari za maeneo ya maziwa nchini.

Akiwasilisha muswada huo jana bungeni, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi, alisema madhumuni ya marekebisho hayo ni kuiwezesha bandari katika Jamhuri ya Muungano kufikia viwango vya kimataifa kiutendaji, kuvutia nchi nyingi zaidi na shehena kubwa za mizigo kutumia bandari za hapa nchini.

Alisema serikali imefanya majadiliano na kamati kuhusu marekebisho ambayo yamependekezwa katika sehemu ya nne na tano na kukubaliana na ushauri wa kamati kwa kuondoa marekebisho hayo.

Alisema ili kutekeleza ushauri huo wa kamati, muswada umefanyiwa marekebisho kupitia jedwali la marekebisho kwa kuondoa sehemu ya nne na tano.

Dk. Feleshi alisema sehemu sita ya muswada huo inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya viwanda sura ya 159. Kifungu cha nne kinachobainisha majukumu ya shirika kinapendekezwa kurekebishwa, ili kuliwezesha shirika kufanya shughuli ambazo zinaendana na maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu uliopo na unaoendelea kutokea duniani.

Pia alisema kifungu cha saba kinapendekeza kurekebishwa ili kupitia shirika mamlaka ya kuanzisha kamati mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zake.

Kifungu cha 12 kinachohusu uratibu wa utafiti zinazofanywa nje ya nchi kinapendekezwa kufutwa kwa kuwa mfumo wa uchumi wa sasa umebadilika na shughuli za utafiti wa viwanda hazisimamiwi na serikali pekee.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Festo Dugange, akijibu maswali ya baadhi ya wabunge katika kikao cha kwanza cha mkutano wa 12 wa Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

**"Kwa kuwa Bunge lilishafanya uamuzi, tusije tukajikuta Bunge letu hili tunarejea tena kwenye kutoa mawazo juu ya jambo hili ambalo tulishafanya uamuzi.**

Kifungu cha 19 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuziwezesha mahakama zenye mamlaka kwenye maeneo husika kusikiliza mashauri yanayotokana na madai yanayohusu ushuru wa bidhaa za viwandani unaotozwa.

"Lengo la marekebisho haya ni kuziwezesha mahakama hizo kusikiliza mashauri tofauti na utaratibu wa sasa ambapo mamlaka hayo yapo chini ya Mahakama ya Hakimu Mkazi pekee," alisema.

Dk. Felesh alisema sehemu ya pili inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Nguvu ya Atomu, Sura ya 188 ambapo kifungu cha 4 inarekebishwa ili kuongeza mawanda ya udhibiti kwa kushusha viwango vya vyanzo mbalimbali vya mionzi vinavyosimamiwa na sheria hiyo.

Alisema lengo la marekebisho hayo ni kudhibiti mmuliko wa mionzi unaotokana na madini ya Viasilia vya Mionzi vya asili (NORMs).

Sehemu ya tatu inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Chuo cha Usafiri wa Majini Dar es Salaam, sura ya 253 na inafanyiwa marekebisho ya jumla ili kuainisha cheo sahihi cha mkuu wa taasisi hiyo kwa kuzingatia matakwa mapya ya NACTVET.

"Lengo la marekebisho haya ni kuendana na matakwa ya utendaji wa taasisi za elimu ambapo Bodi ndiyo inayohusika na uanzishwaji wa vyama vya wanafunzi badala ya waziri," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Joseph Mhagama, alisema kamati inaipongeza serikali kwa kuleta marekebisho kwa kufuta sehemu ya nne na tano ya muswada.

Mhagama alisema marekebisho hayo yanakusudia kuondoa matumizi ya sheria hiyo kwenye masuala ya yanayohusu uendelezaji, uendeshaji au mpango wa mpango wa uendelezaji wa utajiri wa mali za asili endapo utakuwa na lengo la kuboresha ufanisi wa bandari za bahari, bandari kavu na maziwa nchini.

Alisema kwa ujumla marekebisho hayo yanalenga kuhakikisha kuwa utekelezaji wa sheria hizo hauathiri utendaji wa maeneo ya bandari ili kuziwezesha kufikiwa kiwango cha kimataifa kiutendaji.

"Waheshimiwa wabunge muswada umesomwa kwa mara ya tatu na kwa utaratibu tuliojiwekea tumekamilisha utungaji wa sheria kwa maana ya kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali zilizoletwa kwetu. Kwa hivyo muswada wa sheria wa marekebisho mbalimbali namba mbili (2023), umepitishwa rasmi na Bunge," alisema Spika Tulia.

Alisema kwa utaratibu wa Bunge watampelekea Rais ili aweze kufanya yale ambayo Katiba inataka awe ameshiriki ili atie saini kama ataona unafaa na kisha taarifa zitarudishwa bungeni.

## Rais Samia aahidi neema sekta binafsi, akizindua ujenzi miradi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema hakuna maendeleo bila sekta binafsi na serikali itaendelea kujenga mazingira wezeshi na kutoa nafasi kufanya shughuli za maendeleo yanayotegemea pande zote.

Vilevile, ameagiza kuweka wazi motisha zilizopo kwa wawekezaji mbalimbali ili waje wengi kwa faida ya nchi kiuchumi na ajira kwa Watanzania.

Mkuu wa Nchi pia amesema amerekodi filamu nyingine iitwayo 'Karibu Kijiji cha Milele' kwa kushirikiana na Raia wa China, ambayo itatengenezwa kwa lugha ya Kichina na kutafsiriwa kwa Kiswahili. Inatarajiwa kuleta watalii wengi kutoka Asia.

Rais Samia aliyasema hayo jana wakati akizindua rasmi Hoteli ya Kitalii ya Kwanza Resort katika Kijiji cha Kizimkazi visiwani Zanzibar, ambako alikozaliwa.

Alisema ni lazima kubadili mtazamo kwenda kwa kasi na mabadiliko ya dunia na kuona fursa na kujijenga kama wengine walivyofanya ikiwamo kwenye uwekezaji na kushirikiana na sekta binafsi.

"Ninaishukuru sana sekta binafsi kwa kuendelea kuwekeza, pale ambako wanaweza kuweka fedha tujenga mazingira mazuri ili wafanye, nasi tufanye na ile miradi ambayo haiwawezi kama maji na mengine ila huku kwenye hoteli na miradi mingine tuwaachie sekta binafsi.

"Royal tour imeongeza watalii na wengi kupenda kuja kuwekeza, tunawaomba mvute wengine zaidi. Kwa sasa Zanzibar wageni wanatuzidi, hawana pa kulala. Tunapaswa kuwa na hoteli kubwa kwa ajili ya wageni. Kama kuna 'incentives' (motisha) ziwekwe wazi ili sekta binafsi wavutiwe na kuja kujenga hoteli kubwa," aliagiza.

Rais pia alipongeza mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali ya Zanzibar kuvutia wawekezaji kuwekeza katika hoteli ikiwa ni pamoja na kurahisisha utoaji wa huduma za mahitaji muhimu.

Rais alisema ili kuepuka vifo vitokanavyo na uzazi, lazima wajawazito kuvitumia vituo vya afya, ili kujifungua salama wakiwa chini ya uangalizi wa wataalamu wa afya.

Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema kasi ya ujenzi wa vituo vya afya vyenye hadhi ya kutoa huduma kwa wajawazito na watoto kwa kiasi kikubwa itapunguza vifo hivyo.

Rais Samia pia alikabidhi magari mawili kwa ajili ya ulinzi katika Ukanda wa Utalii wa Mkoa wa Kusini Unguja na kusisitiza umuhimu wa kufanyika doria na kuona hakuna matukio yanayotishia usalama wa wageni.

Kamishna wa Jeshi la Polisi, Hamad Khamis Hamad, alisema wamejipanga kuimarisha doria katika maeneo yote ya ukanda huo na maeneo yote ya utalii kuanzia Mkoa wa Kusini Unguja hadi Kaskazini Unguja.

**SKULI YA MIL. 600/-**

Rais Samia pia aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa Skuli ya Maandalizi Tasani, iliyoko Shehia ya Tasani, Makunduchi, inayojengwa na Benki ya NMB. Ujenzi utagharimu Sh. milioni 600 hadi utakapokamilika Desemba mwaka huu.

Akitoa maelezo ya mradi huo kwa Rais Samia, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema ujenzi huo ambao ni sehemu ya Programu ya Uwekezaji kwa Jamii (CSI), ni kati ya jitihada za wazi za benki yake katika kumwunga mkono kufanikisha Sera ya Elimu Bure kwa shule za msingi hadi sekondari nchini.

Zaipuna alimweleza Rais Samia kwamba ujenzi huo utakaojumuisha madarasa matano yatakayochukua wanafunzi 200 kwa mkupuo, utakamilika Desemba mwaka huu, tayari kwa mwaka wa masomo 2024.

"Ujenzi wa majengo na samani za ndani kama vile viti, meza na madawati, utaigharimu benki Sh. milioni 600, ambazo ni sehemu ya faida yetu tunayoitoa kila mwaka kurejesha kwa jamii.

"Mradi huu ulio katika eneo la mita za mraba 467, utajumuisha madarasa matano yatakayobeba wanafunzi 40 kila moja, Ofisi ya Mwalimu Mkuu, Ofisi ya Walimu, jiko, vyoo vya walimu, wafanyakazi na wanafunzi, stoo, mifumo ya kisasa ya maji safi na majitaka, pamoja na sehemu ya michezo.

Rais Samia aliishukuru benki hiyo kwa namna inavyounga mkono jitihada za serikali yake na ile ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuboresha mazingira ya watoto kupata elimu, huku akiweka ahadi ya kurudi Tasani Januari mwakani wakati wa kuzindua shule hiyo.

Tamasha la Kizimkazi linaloambatana na maonesho ya bidhaa mbalimbali, likifanyika chini ya kaulimbiu 'Tuwalinde Kimaadili Watoto Wetu kwa Maslahi ya Taifa'. Lilizinduliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi Agosti 26 na litafungwa na Rais Samia kesho.

Ni tamasha linalotumika kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na wadau zikiwamo taasisi binafsi.




Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Jumanne Muliro, akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu kukamatwa kwa walinzi wa kampuni ya Pasco, askari wa misitu na askari polisi kwa tuhuma za mauaji ya wauza mkaa katika eneo la Kibamba hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# EWURA yajivunia miaka 17 ya mafanikio

**Na Mwandishi Wetu**

MAENDELEO ya kiuchumi katika nchi huletwa na mambo mengi, ikiwamo taasisi za kimaendeleo za serikali na zisizo za kiserikali kuwawezesha wananchi kutambua na kuzitumia vizuri fursa za kiuchumi zilizopo kwenye maeneo yao.

Moja ya taasisi za serikali ambazo zinachangia katika kuleta maendeleo hapa nchini ni mamlaka za usimamizi ambazo zimepewa jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za kiuchumi na kijamii, ili huduma zake zinawafikie wananchi moja kwa moja.

Moja ya Taasisi hizo ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), iliyoanzishwa mwaka 2006 na kupewa dhamana ya kusimamia shughuli za kuchakata, kusafirisha, kusambaza na kuuza mafuta na gesi asilia nchini.

Majukumu makubwa ya mamlaka hiyo ni kutoa leseni za uendeshaji wa shughuli za nishati na maji nchini, mapitio ya ushuru, utendaji wa ufuatiliaji wa viwango, ubora, usalama, afya na mazingira.

EWURA pia ina wajibu wa kukuza na kuendeleza ushindani wenye tija kiuchumi, kulinda maslahi ya walaji pamoja na kuendeleza upatikanaji wa huduma zilizowekwa kwa watumiaji wote wakiwamo wa kipato cha chini, waishio vijijini na wasiostahili katika sekta zilizosimamiwa.

**MAFANIKIO**

Tangu kuanzishwa kwake miaka 17 ilyopita mamlaka hiyo imeleta mabadiliko makubwa katika sekta ya nishati nchini, ikiwamo kudhibiti kupanda bei za mafuta, gesi, maji na umeme kiholela.

Mafanikio mengine yaliyopatikana tangu mamlaka hiyo ni kukomesha wafanyabiashara waliokuwa wakigoma kuuza mafuta wakisubiri yaadimike, ili wapandishe bei, kwa kuwachukuliwa hatua za kisheria wenye tabia hizo.

Meneja wa Ufundi Kitengo cha Mafuta EWURA, Mhandisi Shabani Suleiman, alisema mamlaka hiyo pia imefanya juhudi kubwa kuwadhibiti wafanyabiashara ya mafuta katika vituo bubu na maeneo mengine yasiyoruhusiwa.

"Kufanya hivyo nikinyume cha sheria na adhabu yake ni kulipa faini kiasi kisichozidi milioni tano au kifungo cha miaka mitatu jela,"anasema.

Kuanzishwa kwa EWURA pia kunasukuma taasisi zote kuheshimu sheria, kanuni na taratibu pamoja na kufuata hatua mbalimbali ikiwamo kushirikisha wadau, hususan watumiaji wa bidhaa husika kama vile umeme na maji.

Aidha, ilidhibiti ubora wa mafuta ya petroli kwa kuhakikisha wafanyabiashara ya mafuta wanafuata sheria, kanuni na kukidhi viwango vya ubora katika utoaji huduma za mafuta nchini.

Vilevile mamlaka hiyo inafanya ufuatiliaji kwa umakini kwa uendeshaji wa biashara ya mafuta nchini, ili kuhakikisha huduma inayotolewa inamlinda mtumiaji dhidi ya madhara ya kiafya, kiusalama na kimazingira.

Kwa mujibu wa Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano EWURA, Titus Kaguo, anasema wanaendelea kupunguza athari za matumizi ya gesi asilia kwa wananchi wa maeneo husika na kuwaacha maskini.

Alisema moja ya mbinu wanazozitumia ni kutoa elimu ya vyuo vikuu bure kwa wazawa wenye sifa, ili kuongeza wataalam wa kwenye kada ya gesi asilia, na taarifa za utekelezaji zinasambazwa kila mara miongoni mwa wadau.

'EWURA pia imekuwa ikifanya jitihada kubwa katika kuimarisha mazingira ya kuvutia uwekezaji katika miradi ya umeme ili kushajihisha utekelezaji wa sera ya viwanda," alisema.

Kaguo alisema mamlaka hiyo imekuwa ikihamasisha ushiriki wa sekta binafsi kwenye uwekezaji wa miradi midogo ya kuzalisha umeme chini ya Megawati 10 kwa kuandaa mikataba elekezi ya kuuziana umeme kati ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na wawekezaji.

Alisema mikataba hiyo pamoja na mambo mengine hupunguza muda wa majadiliano kati yao na inawezesha uwekezaji na utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini.

Aidha alisema EWURA imetayarisha bei elekezi za ufuaji umeme utokanao na maji, gesi asilia, makaa ya mawe, jotoardhi, umeme wa jua, upepo na mafuta ili kuiwezesha Tanzania kuwa na umeme wa uhakika kwa matumizi ya viwanda.

Mamlaka hiyo pia imeendelea kuratibu mabadiliko katika sekta ndogo ya umeme (ESI) ambayo yanalenga kuongeza uwezo wa uzalishaji kufikia Megawati 10,000 ifikapo mwaka 2025.

Aidha, katika kutekeleza majukumu yake ya kiudhibiti, EWURA imeboresha huduma za utoaji leseni za umeme kwa kuimarisha mfumo wa uombaji leseni kwa njia ya mtandao (LOIS), upangaji wa bei pamoja na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na kudhibiti mafundi umeme wasio na kibali.

# Kikokotoo mafao wastaafu chaibua hoja bungeni

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KIKOKOTOO cha mafao ya wastaafu kimeendelea kuibua mijadala bungeni baada ya jana baadhi ya wabunge kuitaka serikali kurekebisha kanuni hizo za utoaji mafao ili kuondoa malalamiko ya wastaafu.

Wakati wa kipindi cha 'Maswali' bungeni jijini hapa jana, Mbunge wa Moshi Mjini (CCM), Priscus Tarimo, alihoji mpango wa serikali kushughulikia malalamiko ya wastaafu kuhusu kikokotoo kinachotumika kupiga hesabu na kulipa mafao.

"Kwa kuwa kumekuwapo malalamiko mengi kuhusu kikokotoo hicho na inaonekana hakuna mpango wa kukirekebisha, sasa serikali imejipangaje kuhakikisha hata hicho kiasi kinachotolewa kitolewe kwa wakati?" alihoji.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariam Kisangi, alisema kuna walimu walikumbwa na kanuni hizo wakati wakisubiri mafao yao na hadi sasa mfumo wa pensheni hauko sawa. Akahitaji kauli ya serikali.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Ester Bulaya, alisema malalamiko makubwa ya wastaafu ni mafao ya mkupuo ambayo yametolewa kutoka asilimia 50 hadi 33.

"Mtu aliyetakiwa kulipwa Sh. milioni 100 akistaafu, sasa analipwa Sh. milioni 50 na huo ndio msingi. Lini mtaleta sheria mbadilishe ili wastaafu wapate asilimia 50 wajikimu?" alihoji.

Mbunge wa Sumve (CCM), Kasalali Mageni, alisema kikokotoo ni kwa ajili ya watumishi na wastaafu ambao hawakitaki.

"Lini serikali italeta muswada wa kufuta kikokotoo hiki ambacho kimekuwa kero kwa watumishi na wastaafu hawakitaki?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alisema serikali itaendelea kutoa elimu ya kanuni hizo kwa kuwa faida ni nyingi kushinda hasara zilizokuwapo awali.

"Tutaendelea kutoa elimu na inaonekana ni kutokuwa na picha ya pamoja, tunaona umuhimu wa kutoa elimu kwa wabunge tena ili kusaidia kutoa elimu kwa wanachama wetu na si kuwapotosha," alisema.

Naibu Waziri huyo alibainisha kuwa hadi Juni 30, mwaka huu, wanachama wa mifuko ya pensheni 131,497 na waajiri 5,580 walikuwa wamefikiwa na elimu hiyo.

Alisema elimu hiyo inatolewa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama Vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA).

Katambi alisema mpango wa serikali ni kuendelea kuwaelimisha wananchi hususani waajiri na wanachama wa mifuko hiyo, wakiwamo wastaafu kuhusu faida ya kanuni hizo.

Alieleza kuwa kwa sasa katika mkupuo wa malipo wanufaika asilimia 81 ya wanachama wote na asilimia 19 mafao yao ya kila mwezi yameongezeka kupitia kanuni hizo.

"Katika malipo yale ya kila mwezi kulikuwa kuna asilimia 50 walikuwa wanalipwa, lakini sasa wamefikia asilimia 67 ya malipo. Haya maboresho yametokana na utafiti uliofanyika na utaratibu wa kuunganisha mifuko ya pensheni umeleta tija kubwa," alisema.

Kuhusu mfumo wa mafao kwa walimu, Katambi alisema utaratibu wa kuunganisha mifuko na kuweka uwiano haukuacha kundi lolote nje ikiwamo walimu.

Katika kipindi hicho, Mbunge wa Sikonge (CCM), Joseph Kakunda, pia alihoji mpango wa serikali kumaliza kero za wastaafu, wakiwamo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Katambi, akijibu swali hilo, alisema suala la wastaafu wa Afrika Mashariki lilikuwa la kimahakama na serikali itaendelea kufuatilia maelekezo ya mahakama ili wapate stahiki zao.

## Marais watano kushiriki Mkutano wa Kimataifa Mifumo ya Chakula

**Na Renatha Msungu**

MARAIS kutoka nchi tano barani Afrika wamethibitisha kushiriki katika Mkutano wa Kimataifa wa Mifumo ya Chakula Barani Afrika uliopangwa kufanyika Septemba 5-8 jijini Dar es Salaam.

Kampuni kubwa za kibiashara pia zinatarajiwa kushiriki katika mkutano huo, wenyeji wakibainisha kuwa tayari wamepokea maombi ya wageni zaidi ya 3,000.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya mkutano huo yanayoendelea katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius (JNICC), jijini.

Alitaja marais wanaotarajiwa kushiriki ni kutoka nchi za Kenya, Angola, Msumbiji, Zimbabwe na Zambia.

Mweri alisema kuwa awali walitarajia kupata washiriki 3,000, lakini mpaka sasa idadi ya washiriki imevuka lengo, imebidi waongeze idadi kutokana na washiriki kuendelea kuomba. Lakini leo (jana) mfumo wa uombaji nafasi ya ushiriki unafungwa," alisema Mweri.

Alisema kutakuwa na shughuli mbalimbali ambazo zitafanyika ikiwamo uzinduzi wa kampuni za mbolea ambazo zitakwenda kuwa suluhisho la wakulima nchini.

Kutokana na hilo, Katibu Mkuu huyo alisema kuna haja Watanzania kushiriki mkutano huo ili wajifunza mambo mbalimbali kutoka kwa wageni.

Jovina Lekinao, mmoja wa washiriki kutoka Tanzania waliojisajili, aliipongeza serikali kutokana na kukubali kuwa wenyeji wa mkutano huo. Mkutano unakwenda kuitangaza nchi katika kilimo na kutoa fursa kwa washiriki kujifunza vitu vingi.

Alisema mikutano ya aina hiyo inawapa fursa wakulima na wafanyabiashara kuona namna wanavyoweza kujiendeleza katika sekta ya kilimo kupitia fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali.




Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo ya ujenzi wa skuli ya maandalizi ya Tasani kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (mwenye kipaza sauti), mkoa wa Kusini Unguja jana, baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi huo utakaogharamiwa na benki hiyo. Wa pili kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid na kushoto ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa benki hiyo, Filbert Mponzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia apongeza ujenzi soko la kisasa Kizimkazi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

KATIKA kuendelea kuwezesha jamii inayoizunguka kupitia sera yake ya uwekezaji kwa jamii, Benki ya CRDB inatarajia kujenga soko la kisasa katika Kijiji cha Kizimkazi, Mkoa wa Kusini Unguja, visiwani Zanzibar.

Hafla ya kuweka jiwe la msingi la soko hilo ilifanyika jana katika eneo la Kizimkazi Dimbani ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za Tamasha la Kizimkazi na kuhudhuriwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza wakati wa kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa soko hilo, Rais Samia aliishukuru Benki ya CRDB kwa kukubali ombi la Mkoa wa Kusini kujenga soko hilo la kisasa. Litachochea maendeleo ya watu wa Kizimkazi na Mkoa wa Kusini Unguja kwa ujumla.

"Mwaka jana kama mnakumbuka, mlinipa kilio hiki cha soko la jamii ya Kizimkazi. Sasa mimi nikalitupa mkoa ambako na wao wakalipeleka CRDB na leo (jana) wako hapa kwenye 'field' tayari kuweka jiwe la msingi na ujenzi unaendelea.

"Kwa hiyo, tuwashukuru sana CRDB kwa kutushika mkono katika hilo na haya ndo maendeleo ya Kusini tuliyoyasema na ndiyo madhumuni ya tamasha letu hili la Kizimkazi," alisema Rais Samia.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema kwa kutambua uchumi wa watu wa kusini unategemea sana uvuvi, Benki hiyo chini ya Taasisi yake ya CRDB Bank Foundation, imeamua kuwekeza katika ujenzi wa soko la kisasa ambalo litakwenda kuongeza thamani katika biashara kwa wakazi wa eneo la Kizimkazi.

Katika awamu ya kwanza ya ujenzi wa soko, benki imetenga Sh. milioni 157.8 na tayari ujenzi wa sehemu ya kwanza umeanza.

"Kwa muda mrefu Benki ya CRDB imekuwa mdau mkubwa wa maendeleo ya Kizimkazi kupitia Tamasha la Kizimkazi ambapo hadi kufikia tamasha la mwaka huu, Benki ya CRDB imeshafanya uwekezaji wa takribani Sh. bilioni moja na soko hili la kisasa la samaki litagharimu zaidi ya Sh. bilioni mbili hadi kukamilika kwake. Sehemu ya kwanza ya ujenzi itakamilika mnamo mwezi Oktoba 2023," alisema Nsekela.

Mbali na utoaji wa huduma za fedha kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano, Benk ya CRDB pia imekuwa inatekeleza sera yake ya uwekezaji katika jamii katika pande zote mbili.

Sera hiyo ya uwekezaji katika jamii inaelekeza asilimia moja ya faida kurejeshwa katika jamii katika maeneo ya elimu, afya, mazingira na uwezeshaji kwa wanawake na vijana.

"Mbali na ujenzi wa soko hili la kisasa, benki kupitia taasisi yake ya CRDB Bank Foundation, imeendelea na dhamira yake ya kuleta mageuzi katika mchezo wa Resi za Ngalawa ambapo katika Tamasha la Kizimkazi la mwaka 2023, benki imewekeza zaidi ya Sh. milioni 119.5 katika mashindano ya Resi za Ngalawa ambazo ni sehemu ya Tamasha la Kizimkazi," alisema Nsekela.

Mwaka 2021, Benki ya CRDB ilikuwa mdhamini mkuu wa Tamasha la Kizimkazi kwa kugharamia tamasha lote kuanzia mafunzo kwa wajasiriamali, michezo, maonyesho ya wafanyabiashara hadi kilele cha tamasha. Mbali na hilo, benki ilifadhili ujenzi wa nyumba za madaktari na Ofisi ya Sheha.

Mwaka 2022, Benki ya CRDB ilijenga maabara ya Shule ya Sekondari Kizimkazi na kununua vifaa vyake vya maabara. Sambamba na hilo, benki hiyo ilifadhili michezo yote na zaidi kuleta mapinduzi katika mchezo wa Resi za Ngalawa, ulivutia watu wengi zaidi na kutoa zawadi kubwa zilizobadili maisha ya wana Kizimkazi ikiwamo zawadi kubwa ya boti ya kisasa yenye thamani ya Sh. milioni 30 kwa mshindi.

## Askari polisi sita mbaroni kwa tuhuma za mauaji

**Na Pilly Kigome**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia askari polisi sita, askari 11 wa Kampuni ya Ulinzi ya Pasco Ltd na maofisa wawili wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), kwa tuhuma za kujeruhi na kusababisha vifo vya watu wawili.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa watuhumiwa hao wote wanashikiliwa na jeshi hilo kwa tuhuma hizo.

Muliro alisema tukio hilo lilitokea Agosti 28 mwaka huu saa nane usiku huko Kiluvya, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani.

Alisema majira hayo, askari hao wakiwa katika majukumu yao ya kazi, walikutana na kundi la watu wapatao 30 wakiwa na pikipiki huku wamebeba mkaa. Waliwasimamisha, lakini hawakutii amri ya polisi.

Inadaiwa watu hao walianza kukimbia na kutelekeza pikipiki hizo na baadaye walirudi wakiwarushia mawe askari hao.

"Ndipo askari hao wakaanza kufyatua risasi zilizopelekea watu wawili kujeruhiwa na baadaye kupoteza maisha.

"Jeshi la Polisi Kanda Maalum likafika eneo hilo mara baada ya kupata taarifa hiyo na uchunguzi wa kina unaendelea kwa kushirikiana na vyombo vingine vya kiuchunguzi huku tukiwashikilia askari hao.

"Hatutamwacha mtu ambaye atabainika ni mhalifu katika tukio hilo. Jeshi letu halivumilii vitendo vya uhalifu," alisema Muliro.

Alisema miili ya watu hao imehifadhiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila. Waliofariki dunia hawajatambuliwa kwa majina.

Mnamo tarehe 15 Julai mwaka huu, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu madhila yanayowakumba wasafirishaji wa mkaa kwa pikipiki katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, hata kufikia hatua ya kushikiwa mtutu na askari wa TFS.

# Watumishi wa Mahakama Kuu wafikishwa kortini madai kutafuna fedha za mirathi

**Na Abdallah Bakari,**
MTWARA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mtwara, imewafikisha mahakamani watumishi watatu wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara kwa mashtaka 19 ya uhujumu uchumi.

Watumishi waliofikishwa kizimbani ni wahasibu Beda Nyasira na Theodosia Mtelani na mtunza kumbukumbu Mahafudhi Chinenda, ambao ni watumishi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara. Watumishi hao wanashtakiwa kwa ubadhilifu wa Sh. 56,663,213.24 za mirathi.

Akiwasomea mashtaka yanayowakabili, Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU, Naftali Mnzava, aliiambia Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa Mtwara mbele ya Hakimu Mkazi wa Mfawidhi, Fredrick Mnzava, kuwa washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2022.

Katika kipindi hicho, alidai kuwa washtakiwa walijipatia fedha kutoka kwenye akaunti ya mirathi ya Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara ambazo zilikuwa zitumike kuwalipa warithi, lakini wakazipindisha.

Alidai kuwa katika kesi hiyo Na. 4 ya mwaka 2023 ya uhujumu uchumi, watumishi hao wanashtakiwa kwa mambo manne yaliyogawanyika katika sehemu 19.

Mnzava aliyataja mambo hayo makuu kuwa ni pamoja na matumizi mabaya ya madaraka, kujipatia fedha kwa njia isiyo ya halali, utakatishaji wa fedha na kuitia serikali hasara.

"Matumizi mabaya ya madaraka, kujipatia fedha kwa njia isiyo ya halali na utakatishaji wa fedha haya ni makosa matatu yanayojitegemea na hili la kuitia mamlaka hasara limegawanyika katika makosa mengine 16, hivyo kufanya jumla ya mashtaka yao kuwa 19. Makosa yote yanaangukia chini ya Sheria ya Uhujumu Uchumi" alidai Mnzava

Washtakiwa hao wanaotetewa na Wakili Alex Msolenge, walikana mashtaka lakini dhamana yao imezuiwa kutokana na mashtaka yao kutokuwa na dhamana, hivyo walirejeshwa rumande.

Hakimu Mnzava aliihairisha kesi hiyo hadi Septemba 11, mwaka huu kesi hiyo itakapoanza kusikilizwa.

Julai 14, mwaka huu, gazeti hili liliibua ubadhilifu wa Sh. milioni 695. 5 katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2022 katika Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya Mtwara uliofanywa na baadhi ya watumishi wa ofisi hiyo.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (kushoto), akipata maelezo ya upanúzi wa mtambo wa uzalishaji maji Wami kutoka kwa Meneja wa mtambo huo, Mhandisi Emaculata Msilama (kulia), alipofanya zíara kwenye mradi wa Chalinze awamu ya tatu, mkoani Pwani jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wananchi kuunganishiwa maji kwa mkopo

**Na Joseph Mwendapole**

NAIBU Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuwaunganisha wanufaika wa Mradi wa Maji Chalinze Awamu ya Tatu na huduma ya majisafi kwa mkopo baada ya kukamilika kwa mradi huo.

Aliagiza hayo jana alipozungumza na wananchi wa Kijiji cha Kihangaiko, Kata ya Msata, Halmashauri ya Chalinze, Wilaya ya Bagamoyo wakati wa mkutano wa hadhara baada ya ziara ya kukagua upanuzi wa mtambo wa kuzalisha maji wa Wami.

"Kwanza kabisa, ninamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza jitihada za kuhakikisha adhma ya kumtua mama ndoo kichwani inafanyika kwa vitendo. Pia niwapongeze watendaji wa DAWASA, hakika kazi ya utekelezaji wa mradi huu ni nzuri na inaonekana!" Alipongeza.

Aliagiza DAWASA kuwaunganisha wanufaika wa mradi huo kwa mkopo kwa kuzingatia masharti nafuu na vigezo rafiki ili kila mwananchi apate huduma ya majisafi karibu na makazi yake.

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okashi, alipongeza Wizara ya Maji kwa kusimamia vyema utekelezaji wa miradi ya maji katika Wilaya ya Bagamoyo hususani Mradi wa Maji Chalinze Awamu ya Tatu.

Alisema mradi huo ni muhimu kwa kuwa unakwenda kuondoa changamoto ya upatikanaji wa maji iliyokuwapo kwa muda mrefu.

"Tutakuwa wachoyo wa fadhila kama tutaacha kumshukuru Rais wetu msikivu ambaye kwa namna kubwa ametusaidia wanawake wa Wilaya ya Bagamoyo sasa upatikanaji ni wa uhakika.

"Pia tunawapongeza DAWASA kwa kuendelea kuipa ushirikiano ofisi yangu ambao tumezunguka nao katika kata zote 26 kusikiliza na kutatua changamoto za wananchi wa wilaya ya Bagamoyo," alisema Okashi.

Akizungumza kwa niaba ya Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Shabani Mkwanywe, alisema mradi huo ni miongoni mwa miradi ya mfano ya vijijini kutokana na usanifu mzuri uliofanyika. Utanufaisha vijiji 59 vya Pwani, Morogoro Vijijini na Wilaya ya Handeni mkoani Tanga.

"Mradi huu wa maji umehusisha upanuzi wa mtambo wa kuzalisha maji Wami, ulazaji wa bomba za inchi 12 na 16 kwa umbali wa kilomita 24, ujenzi wa matangi ya kuhifadhi maji ya chini na juu 19 na ujenzi wa visima vya kuchotea maji 351. Umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 44 na unatarajia kunufaisha wakazi zaidi ya 200,000," alisema Mkwanywe.

Diwani wa Msata, Celestin Mcholo, aliishukuru serikali kupitia DAWASA kuwaletea mradi mkubwa wa maji ambao umeleta mabadiliko makubwa.

Vilevile, alimshukuru Naibu Waziri kwa kupokea kilio chao cha kuunganishiwa maji kwa mkopo.

Aliwaomba wananchi wa Kata ya Msata kutunza miundombinu na vyanzo vya maji ili kuendelea kupata huduma ya maji safi bila changamoto yoyote.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Tahadhari ichukuliwe matumizi ya dawa katika uzazi wa mpango*

**MPANGO** wa uzazi uliasisiwa kwa lengo la kupunguza uzazi usio na mpangilio ili kujenga familia na jamii yenye afya njema pamoja na kuziwezesha mamlaka mbalimbali kuwa na mipango thabiti ya maendeleo. Moja ya njia ambazo zimeshauri ni wanafamilia kupanga uzazi kwa kutofautisha muda kati ya mtoto mmoja na mwingine.

Hatua hiyo ilitokana na utafiti na uhalisia katika familia nyingi kutokujali namna ya kuzaa watoto na matokeo yake kwenye jamii nyingi watoto walikuwa wakizaliwa kila mwaka.

Kwa hali hiyo uzazi wa mpango haukutiliwa maanani huku baadhi ya watu wakidai kuwa ni rukhsa kuzaa kadri uwezavyo kwa kuwa kila mtoto anakuja na riziki yake.

Kutokana na hali hiyo, takriban miaka 15 hadi 20 iliyopita, lilikuwa jambo la kawaida katika familia kuwa na watoto 10 na zaidi huku wakiwa wamepishana kwa wastani wa mwaka. Hali hiyo ilisababisha hali ya afya ya mama na mtoto kudorora kutokana na kuzaa mfululizo na pia mtoto kutokupata chakula kinashostahili katika makuzi yake hususan maziwa ya mama. Kwa kawaida, mama anapozaa mfululizo anapata madhara ya kiafya huku mtoto naye akikua katika njia siziso sahihi na kusababisha udumavu na utapiamlo.

Baada ya utafiti na hali halisi katika jamii, serikali kwa kushirikiana na taasisi za ndani na nje, likiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), ilianzisha kampeni ya uzazi wa mpango ambayo ilisisitiza angalau mama kupata ujauzito baada ya kumaliza miaka miwili tangu mtoto aliyetangulia kuzaliwa.

Ili kufanikisha hilo, baadhi ya njia za uzazi wa mpango zilipendekezwa zikiwamo matumizi ya dawa za kuzuia ujauzito, matumizi ya kondomu kama kinga dhidi ya ujauzito na maradhi yatokanayo na kujamiana, kuweka kijiti au kitanzi kwa mwanamke hasa kama hawawezi kufuata majira kulingana na mzunguko wa hedhi.

Hivi karibuni kwa mfano, imebainika kuwa baadhi ya wanawake hasa mabinti ambao wamekuwa wakishiriki vitendo vya ngono, hawatumii kinga dhidi ya ujauzito na baadhi yao wamekuwa wakipata ujauzito na kutoa kwa kutumia dawa mbalimbali zikiwamo 'Flagyl'.

Mabinti hao wakiwamo wasomi, baadhi wamebainika kununua dawa hizo na kujipangia namna ya kuzitumia, kwa kumeza vidonge tisa ndani ya saa chache. Kutokana na hali hiyo, mabinti hao wameonywa kuhusu madhara ya matumizi ya dawa hizo kwamba husababisha kuathiri uoni na mwili kupata ganzi.

Daktari Bingwa wa Uzazi kukatika Idara ya Uzazi Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala (MRRH), Mugalu Kitandu, akizungumza katika mafunzo ya kuhamasisha vyombo vya habari kujikita kwenye uandishi wa habari za afya ya uzazi na uzazi wa mpango, aliweka bayana kuwa hivi sasa kumekuwa na ongezeko la matumizi holela ya dawa hiyo, hasa kwa mabinti waliopo masomoni ambao wamekuwa wakinunua katika maduka ya dawa flagyl bila mwongozo wa wataalamu wa afya, kwa madai ya kuhofia kupata ujauzito.

Dk. Kitandu alibainisha kuwa mbali na matumizi ya P2 kuwa makubwa kama ambavyo hata Waziri wa Afya imebainisha mara kwa mara, wasichana wamekuwa wakimeza dawa hiyo kabla na baada ya tendo la ndoa kwa ajili ya kujikinga na mimba wakiamini kuwa kwa kufanya hivyo inasafisha kizazi.

Ni wakati mwafaka sasa elimu kuhusu mpango wa uzazi, ikiwamo matumizi ya dawa mbalimbali katika kujikinga na ujauzito kutolewa. Elimu hii ni muhimu kwa vijana kuanzia shuleni ili watambue njia bora za matumizi ya uzazi wa mpango pamoja na madhara yatokanayo na dawa mbalimbali sahihi katika azma hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# *Wazazi, walezi saidieni ukatili shuleni uishe*

**VITENDO** vya baadhi ya wanafunzi kufanyiana ukatili wa kijinsia kwa kuhusisha ngono kinyume cha maumbile vinasikika kote, shuleni na mitaani, hali inayotishia mustakabali wa masomo.

Vitendo hivyo vimekuwa havizungumziki kirahisi ukilinganisha na ukatili mwingine kama vile ubakaji na hivyo kusababisha viendelee kushamiri.

Taarifa mbalimbali za wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia, zinaeleza kuwa matukio hayo hutokea kwenye mazingira yanayofahamika kuanzia shuleni mitaani hadi nyumbani.

Kushamiri kwa vitendo hivyo, kumelifanya shirika la Himza Development Organization (HDO), kuanza kuzunguka kata hadi kata Dar es Salaam kufundisha wazazi na walezi elimu ya malezi bora.

Ni wiki iliyopita lilikuwa katika kata ya Mbagala Kuu, likitoa elimu hiyo kwa wazazi na walezi, huku wakitakiwa kujua marafiki wa watoto wao shuleni na pia kuwa karibu na walimu.

Mbali na hilo, wanahimizwa kufutilia maendeleo ya watoto wa shuleni ili kupata taarifa mbalimbali zinazowahusu, lakini pia wanajenga urafiki na watoto wao ili kama wana jambo linawasumbua, basi waweze kuwaeleza.

Yapo mengi ambayo yalizungumzwa katika mafunzo hayo, ambayo ni utaratibu kwani ni muhimu kupingana na ukatili huo, na ukweli ni kwamba tatizo la ulawiti kwa watoto linakua kwa kasi.

Wazazi na walezi wana kazi kubwa ya kuwafuatilia na kuwachunguza watoto wao, kila mmoja ana wajibu wa kuokoa kizazi cha sasa na cha baadaye kwa kuzingatia usimamizi na ufuatiliaji wa mienendo yao.

Ninaamini kwamba walimu wa shule za msingi na sekondari kwa upande wao, wanafuatilia kwa ukaribu wanafunzi, lakini wakikosa ushirikiano kutoka kwa wazazi na walezi hali inayoweza kuendelea kuwa mbaya.

Mkurugenzi wa Himiza Development Organization, Prisca Ngwesheni, anaeleza kuwa amewahi kufuatilia katika shule mbalimbali na kubaini kuwa wanafunzi hujifuanza mambo hayo kupitia simu.

"Hizo simu ni za kaka zao au watu wengine wa mitaani, hivyo ni muhimu, wazazi na walezi tuwe karibu na watoto wetu tuwafanye marafiki tuwasikilize, tuwahoji watakuwa wazi," anasema Prisca.

Aidha, Prisca anabainisha ukweli huo, ambao ni jambo la muhimu sasa kwa kila mzazi na mlezi kufanya sehemu yake katika malezi na pia kuwa karibu na walimu ili kupata taarifa za maendeleo ya watoto wao shuleni.

Kwa njia hiyo, inaweza kuwa rahisi kwao kujua chochote kuhusu watoto hao badala ya kuachia walimu kila kitu, kwani mtoto anaweza kutoka shuleni mapema na kuishia mitaani kwenye vitendo hivyo.

Lakini pia anaweza kufanyiwa shuleni au yeye akafanyiwa na wenzake shuleni, kwani inaelezwa wanafunzi wanafanyiana vitendo katika vyoo vya shule au katika majengo ya madarasa ambayo hayajakamilika.

Wasichana nao inaelezwa kuwa wanakumbana na ukatili huo wa kijinsia kutoka kwa walimu wao wanaowataka kingono, wanapokataliwa ndipo hufanyiwa visa kama kuchapwa bila sababu, kupewa alama ndogo, adhabu ngumu au kutishiwa kufukuzwa shule.

Ingawa wanafunzi wa kike wanatakiwa kujua mbinu mbalimbali za kuzuia vitendo vya ukatili, lakini pia wawe tayari kutoa taarifa kwa wazazi, walezi na walimu wengine au vyombo dola.

Hilo litawezekana iwapo watakuwa wamejengewa mazingira ya kuwa huru kutoa taarifa hizo, lakini kama wazazi, walezi na walimu watakuwa wakali, itakuwa vigumu wanafunzi kueleza yanayowasibu.

Kwa ujumla, vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyofanyika shuleni iwe ni wanafunzi kwa wanafunzi au kufanyiwa na walimu wao, vina matokeo mabaya katika elimu.

# Ahukumiwa kulipa 200,000/- kukata tiketi bila kulipia

**Na Waandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Mwanzo Kariakoo imemhukumu Edward Nyerere (35), kulipa faini ya Sh. 200,000 au kwenda jela miezi mitatu, baada ya kukutwa na hatia ya kukata tiketi ya ndege kwenda China bila kufanya malipo.

Hukumu hii ilitolewa jana na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Kariakoo, Claudis Kipande, baada ya kuridhika na ushahidi uliotolewa mahakamani kuwa mshtakiwa alikata tiketi hiyo kupitia wakala Waheguru Travelling yenye thamani ya Sh. milioni tano bila kufanya malipo.

"Mahakama imekukuta na hatia, hivyo utatakiwa kulipa faini ya Sh. 200,000 au kifungo cha miezi mitatu jela na kulipa gharama za tiketi hiyo kwa Ofisa Masoko wa Wakala, Jamila Kawawa, kama fidia ya fedha aliyotumia kukata tiketi," alisema Hakimu.

Hukumu hiyo ilitolewa baada ya mshtakiwa kukiri kosa lililofanyika Mei 15, mwaka huu, majira ya saa 8:00 mchana katika jengo la Diamond Plaza, wilayani Ilala, kwa kukata tiketi na kutoweka bila kulipa.

Mshtakiwa alifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza kwa madai ya kujipatia huduma kwa njia ya udanganyifu na kukataa kosa hilo na baadaye kukubali shtaka lilomkabili kinyume cha sheria.

Wakati huo huo, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeahirisha kesi ya kukutwa na dawa za kulevya aina ya Cannabia Sativa kilo 10.05 inayomkabilia Alfani Omari (23).

Mbele ya Hakimu Mkazi Evodia Kyaruzi, Wakili wa Serikali, Winniwa Samson, alidai kuwa mshtakiwa huyo alikamatwa Juni 20, mwaka huu, eneo la Posta ya Zamani wilaya ya Ilala.

Aliiomba mahakama kumpa tarehe nyingine ya kumsomea maelezo ya awali, ombi lililokubaliwa na hakimu na kupanga kusikilizwa Septemba 11, mwaka huu.

**Imeandikwa na Khadija Kategile (TUDARCo), Gifty Kenny (UDSM) na Salma Chindole (SAUT)**


## FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED

1st Housing

**FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED** commenced its operations in October 2017 as a fully-fledged financial institution specializing on the provision of residential mortgages. The company was licensed by Bank of Tanzania in July 2017 to commerce housing finance business under the provisions of The Banking and Financial Institutions Act, 2006 (Cap. 342. R.E. 2002).

We are looking to hire a talented Risk and Compliance Manager to join our team. If you're hard-working and dedicated, First Housing Finance is a great place to grow your career. We are looking for an experienced Risk and Compliance Manager to review our existing and develop and implement new risk management policies. In this role, you will work to identify risks that could impair our reputation, information security, or general operations and suggest ways to mitigate or eliminate them entirely. You will ensure that our company remains fully compliant with relevant policies and Bank of Tanzania regulations. As a Risk and Compliance Manager, you'll be expected to show strong leadership and organizational skills and have expert-level knowledge of applicable compliance practices. You also need to have prior experience working in Risk Management or a compliance-related role.

As Risk and compliance manager, you shall be able to support in the identification and effective management of risks to the mortgage loan origination, processing, sanction, disbursement, portfolio & document management and customer service, and ensuring that effective control environment exists and actively managed in order to reduce operational losses and improve Business-Operating Effectiveness.

**Job Title:** Risk and Compliance Manager
**Reporting to:** Chief Executive Officer
**Location:** Dar Es Salaam

**Duties & Responsibilities – Risk and Compliance Manager**
- To assume overall responsibility for the mortgage loan portfolio with minimal risk and ensure highest quality of the process standards and compliances at all times, including critical oversight of all aspects of credit & operations management.
- To track, monitor, escalate and report deficiencies at any time that may cause loss to the company.
- To submit prescribed reports at monthly, quarterly or at any such periodicity as may be called upon to the management, Board committees, as per the mortgage policy or whenever called upon by the management and Board Committees to do so.
- To develop structures/framework for the population of losses/loss events.
- Presentation of risk based reports on various products, processes, activities, systems and external events to management.
- Development of structures for establishment of the risk appetite for the company, setting of risk tolerance limits and key risk indicators.
- Develop & maintain an effective relationship at the appropriate level with the Business with a view to embedding effective risk management processes.
- Ensure regular dialogue with senior management to review the current risk profile for their business area.
- Provide guidance and support to the Business in raising awareness and understanding of operational risk and governance. This may involve making presentations/training sessions to staff, as well as coaching and informal training as required.
- Provide guidance and support to the Business in advance of internal (and occasional external) audits.
- Any other duties as may be assigned by your supervisor.

**Work Experience and Skills**
- University Degree (Bachelor's) in Finance; Banking, Accounting, Business Administration/Commerce, Economics or related discipline, preferably with other related professional qualifications.
- Formal qualification such as, CPA, CIA, CRMP, is an added advantage.
- Risk management and control techniques (e.g. Risk assessment, auditing, control design)
- Communication and influencing skills, involving staff at all levels of seniority
- Facilitation skills
- Analytical and problem solving skills
- Service excellence
- Good time management and organizational skills
- Team player

**Applications: Qualified candidates to Send CV and application letter to:info@firsthousing.co.tz**

**Deadline: Monday - 04th September 2023 at 05:00pm.**



## FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED

1st Housing

**FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED** commenced its operations in October 2017 as a fully-fledged financial institution specializing on the provision of residential mortgages. The company was licensed by Bank of Tanzania in July 2017 to commerce housing finance business under the provisions of The Banking and Financial Institutions Act, 2006 (Cap. 342. R.E. 2002).

We are looking to hire a talented ICT Manager to join our team. ICT manager shall assist the company employees on day to day running and support of the ICT systems. Leveraging optimal computer technology to the company needs and champion optimal Information Communication Technology systems and projects.

Generally, ICT Manager shall be required to plan, coordinate, and direct computer-related activities in the company. Responsible in determining the information technology goals of the company and responsible for implementing computer software and hardware systems to meet the short and long term goals.

**Job Title:** ICT Manager
**Reporting to:** Chief Executive Officer
**Location:** Dar Es Salaam

**Duties & Responsibilities – ICT Manager**
- Assume management responsibility for Business Contingency planning efforts with a major focus on assuring the adequacy of business unit contingency plans for critical business areas, functions and applications;
- To maintain continued operations, asset protection and loss mitigation in the event of a disruption, coordinating activities of technology resources with the company's business units and development groups, as required;
- Work with business unit management to enhance contingency plans, mitigating the effect of a technology system or application failure or problem. Key objectives are that business units can continue to manage the firm's assets, satisfy our regulatory obligations and maintain our presence in the market place;
- Provide direct communications between the BCP Project Office, Information technology Operations, Technology architecture and Engineering Systems and Systems Application Program Management;
- Assist the department in enhancing, formalizing and standardizing the business planning process, including forecasting and tracking mechanisms, across all business units, to facilitate timely accommodation of future company recovery requirements and opportunities;
- Assume leadership role in developing, coordinating and maintaining comprehensive business contingency plans and validation methodology, to ensure the firm's ability to recovery, in the event of an unforeseen disruption to facilities, technology systems, or applications;
- Perform risk analysis for corporate functional areas to identify points of vulnerability and recommends disaster avoidance and reduction strategies;
- Analyze environmental and equipment configurations for critical corporate resources; recommends disaster avoidance measures and improved backup capabilities;
- Conduct business impact analyses and assist company units to determine critical business processes, identify acceptable recovery time periods and establishes resources required for the successful resumption of business operations in the event of a disaster;
- Assure records required for recovery are identified and properly maintained in the Vital Records Program;
- Coordinate the efforts of staff members in different functional areas in the development of procedures for the continuity of business processes in a disaster situation;
- Establish disaster recovery testing methodologies; plans and coordinate the testing of recovery support and business resumption procedures in different functional areas;
- Assure that recovery procedures are effective for the restoration of key corporate resources and for the resumption of critical business processes;
- Conduct disaster recovery training for staff members in all functional areas. Provide instructional and informational materials on how staffs are expected to respond during an emergency.
- Assist divisions in the assignment and training of staff. Develops and maintains standards and procedures for disaster recovery documentation. Maintain a library of recovery support and business resumption procedures;
- Develop corporate emergency response procedures; distributes and update emergency procedures to reflect changes in staff size, location, organization and home office facilities.
- Monitor the effectiveness of procedures during evacuation drills and revise the procedures as necessary. Maintain a library of emergency response procedures;
- Assist recovery support and business resumption staff during a disaster in the implementation of response and alternate operating strategies;
- Act as a coordinator during an emergency situation;
- Work with vendors of disaster recovery services and facilities; studies and recommend outside services for use during a disaster situation;
- Work with management to ensure that as new equipment, facilities, services and systems are installed that the disaster recovery issues are addressed;
- Work with senior management, Information Technology personnel and outside resources to design and develop effective disaster recovery and business continuity plans;
- Maintain contact with outside contingency planning professional organizations and local/regional emergency response groups;
- Define and manage an effective data backup and retention policy consistent with company recovery needs and manage all system back-up and restore protocol;
- Maintain an updated knowledge of company's board policy, administrative regulations and legal requirements that relate to DR strategy, security of data and copyright laws.

**Work Experience and Skills**
- Bachelor's degree in Computer Science, Information Technology, or a related field
- At least 5 years working experience in ICT management. Similar time being part of a business management team will be an advantage.
- Professional qualifications in systems administration, implementation, and development will be added advantage.
- Project Management skills

**Applications: Qualified candidates to Send CV and application letter to: info@firsthousing.co.tz**

**Deadline: Monday - 04th September 2023 at 05:00pm**

HABARI KITAIFA




Wachakataji wa bidhaa za nyuki, wafanyabiashara na wafugaji nyuki waliochini ya mradi wa kuwezesha mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki (BEVAC), wakipata elimu ya uboreshaji endelevu wa mbinu wakati wa karakana ya mafunzo iliyofanywa na Kituo cha Kimataifa cha Biashara (ITC) jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UCHAMBUZI RIPOTI YA CAG

# Hospitali za Rufani za Mikoa 20 hazikutoa huduma stahiki

**Na Mwanahamisi Mussa,**
TUDARCo

TAASISI ya WAJIBU imechambua ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi (CAG) kwa mwaka 2021/22, ikiainisha dosari kadhaa, zikijumuisha hospitali 20 za rufani za mikoa kutotoa huduma stahiki kwa wagonjwa.

Lengo Na. 3 la Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDG) linahimiza kuhakikisha afya njema na ustawi wa watu wa rika zote.

Vilevile, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2022/26) unakusudia kuimarisha mifumo ya usimamizi upatikanaji na utoaji wa huduma za afya.

Kwa mwaka wa fedha 2021/22, serikali ilitenga jumla ya Sh. trilioni 2.02 sawa na asilimia 5.5 ya Bajeti ya Serikali kutekeleza maeneo ya vipaumbele katika sekta ya afya.

Vipaumbele hivyo ni pamoja na: Kuboresha huduma na miundombinu ya afya katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya; kuboresha huduma za tiba na miundombinu katika hospitali za rufani ngazi ya kanda na taifa; kuboresha huduma za kinga ikiwamo ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba, vitenganishi na chanjo na kugharamia shughuli za utawala na rasilimali watu katika utoaji huduma za afya.

Taasisi hiyo inasema serikali imefanikisha maendeleo katika huduma mbalimbali za afya ikiwamo ununuzi na usambazaji wa vidonge vya uzazi wa mpango, ongezeko la idadi ya wanawake wajawazito katika kliniki na upatikanaji wa huduma bora za afya.

Pia kwa mwaka 2021/22, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, iliratibu ujenzi na ukarabati mkubwa wa vituo vya Afya 304. Kwa kufanya hivyo iliongeza usajili wa vituo vya kutolea huduma za afya nchini kutoka 8,458 kwa mwaka 2020 hadi kufikia 8,549 kwa mwaka 2021. Kati ya hivyo vituo vya kutolea huduma ya afya nchini, hospitali ni 404, vituo vya afya 956 na zahanati 7,1895.

Hata hivyo, ripoti ya CAG kwa mwaka 2021/22 inaonesha upungufu mbalimbali katika utoaji huduma bora za afya katika ngazi ya mkoa na halmashauri. Upungufu huo unajumuisha utoaji huduma usioridhisha katika Hospitali za Rufani za Mikoa: Hospitali 20 hazikutoa huduma stahiki za rufani kwa wagonjwa kutokana na uhaba wa madaktari na vifaa tiba maalum.

Ni hali ambayo CAG anaitaja ilichangiwa na kutotumika kwa baadhi ya vifaa tiba kutokana na matatizo ya kiufundi, kukosekana wataalamu pamoja na uhaba wa majengo.

"Mfano, kutotumika kwa vifaa tiba katika hospitali za rufani za mikoa vyenye thamani ya Sh. bilioni 4.56.

"Pia kutotumika kwa miradi ya afya iliyokamilika yenye thamani ya Sh. bilioni 4.93 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 16 kwa muda wa miezi mitatu hadi miaka mitatu. Miradi hiyo inahusisha zahanati, jengo la wagonjwa wa nje, maabara na kituo cha afya.

"Changamoto hii ilisababishwa na ukosefu wa vifaa tiba, ukosefu wa wafanyakazi na miundombinu rafiki," taasisi hiyo inaorodhesha katika uchambuzi wake.

Pia inautaja upungufu katika utunzaji dawa zilizokwisha muda wake, Mamlaka 16 za Serikali za Mtaa zikiripotiwa kuwa na dawa na bidhaa za afya zenye thamani ya Sh. milioni 976.58 ambazo muda wake wa matumizi umeshaisha kwa kipindi cha kuanzia miezi mitatu hadi miaka 10, lakini hazikuwa zimeteketezwa.

"Pamoja na kwamba CAG hajabainisha sababu zilizokwamisha uteketezaji wa dawa hizo, serikali inapaswa kueleza ni kwa sababu gani dawa hizo hazijateketezwa, kwa kuwa kuwapo dawa hizo kunaweza kuleta madhara," inashauri taasisi hiyo.

WAJIBU inasema katika uchambuzi wake kwamba upungufu uliobainishwa, unaweza kusababisha kuongezeka idadi ya vifo vya wajawazito.

Ripoti ya CAG imeonesha ongezeko la idadi ya vifo vya wajawazito zaidi ya lengo la vifo 100 kwa kila vizazi hai 100,000 katika Mamlaka 20 za Serikali za Mitaa.

"Kutotumika kwa vifaa tiba kwa muda mrefu, kunaweza kusababisha vifaa hivyo kupitwa na wakati, hivyo kutofaa kutumika tena kutokana na maendeleo ya kiteknolojia.

"Miradi kukamilika na kutokutumika kunawanyima wananchi fursa ya kupata huduma stahiki za afya. Hali hiyo inasababisha kukosekana thamani ya fedha ya uwekezaji wa serikali na wadau wa maendeleo.

"Kuendelea kuhifadhi dawa zilizokwisha muda wa matumizi bila kuziteketeza kunaweza kusababisha madhara ya afya kwa umma.

"Mathalani, dawa hizo zikifika mikononi mwa watu wasio waaminifu, zinaweza kuuzwa kwa wananchi na kuleta madhara kwa afya za watumiaji," taasisi hiyo inatahadharisha.

Kutokana na dosari hizo, WAJIBU inapendekeza hospitali za rufani za mikoa, vituo vya afya na zahanati zifanye ununuzi wa vifaa baada ya kubaini mahitaji yao halisi na kuzingatia masuala ya kimazingira na kiteknolojia.

Taasisi hiyo pia inapendekeza Wizara ya Afya kwa kushirikiana na uongozi wa hospitali, vituo vya afya na zahanati husika, kuwa na mikakati itakayohakikisha miradi iliyokamilika inatumika kwa kuajiri wataalamu wenye uwezo wa kutumia vifaa vya afya vya kidigitali na kununua vifaa tiba.

"Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika zichukue hatua stahiki ili kuhakikisha miradi yote iliyokamilika inatumika, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na kupata thamani ya fedha iliyotumika katika ujenzi wa miradi hiyo," taasisi hiyo inahitimisha.

## Vibali kemikali uchimbaji madini vyaongezeka

**Na Mary Geofrey**

MKEMIA Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, amesema kutokana na kuongezeka kwa shughuli za uchimbaji madini nchini, vibali vya kuingiza kemikali nchini vimeongezeka kutoka tani 3,941.73 mwaka 2019 hadi 12,408.89 mwaka 2022.

Dk. Mafumiko aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizindua programu ya utoaji elimu kwa umma, kuhusu kemikali aina ya Sodium Cyanide katika vituo 14 na mikoa minane nchini inayotekelezwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Kanda ya Mashariki kwa kushirikiana na Geita Gold Mining Ltd na Kampuni ya Primefuels ltd.

Alisema mwaka 2020 waliingiza tani 9,092.96 na mwaka 2021 tani 14,408.73 kutoka nje ya nchi ambazo zinaingia kupitia Bandari ya Dar es Salaam na kusambazwa katika mikoa mbalimbali nchini.


"Kupitia mafunzo mnayokwenda kuyatoa, mnakwenda kuyafikia makundi muhimu kwa kuyapa elimu na kuyajengea uelewa wa namna ya kuzuia, kujikinga na kujiokoa endapo kutatokea hatari yoyote inayotokana na kemikali hii hasa pale ambapo kutatokea ajali. Makundi mnayotarajiwa kuyafikia, yatapata elimu sahihi kulingana na wigo wa majukumu wanayosimamia na kuhusika pale linapotokea tukio lolote lenye kuleta hali hatarishi," alisema Dk. Mafumiko.

Alifafanua kuwa Jeshi la Polisi watapata uelewa wa kuchukua maamuzi sahihi wakati wa kuyasimamisha magari barabarani pamoja na ukamataji na uhifadhi wa vielelezo vya kemikali.

Alisema waganga na wahudumu wa afya kwenye hospitali mbalimbali watajengewa uelewa na uwezo wa kujiandaa na majanga, ikiwamo vifaa tiba na dawa sahihi zinazohitajika wakati wa kuhudumia umma ulioathirika na dharura yoyote inayohusisha kemikali ya Sodium Cyanide.

Dk. Mafumiko alisema wananchi wa kawaida waliopo pembezoni mwa barabara na maeneo mengine hatarishi watajengewa uelewa wa kutambua na kuelewa kemikali husika pamoja na madhara yake, hatua za kujikinga na njia za kusaidia waathirika kabla ya kufikishwa vituo vya afya.

Alisema wanatoa elimu kwasababu Sheria ya Kemikali za Viwandani na Nyumbani, Sheria Na. 3 ya mwaka 2003 ya Usimamizi na Udhibiti na Kanuni zake zilizofanyiwa mapitio mwaka 2020, imebainisha makundi mbalimbali ya kemikali zinazosimamiwa ikiwamo ya Sodium Cyanide.



## Wamasai waomba radhi tukio waandishi kushambuliwa

**Na Allan Isaack,**
NGORONGORO

BAADHI ya wafugaji wa jamii ya Kimasai wanaoishi ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, wamelaani tukio la kushambuliwa kwa waandishi wa habari waliokuwa wakitoa elimu katika Kata ya Enduleni.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti juzi, wakati wa mkutano wa mila na upatanisho, Lengai Ngweshie kutoka Kijiji cha Kapenjiro, alisema jamii hiyo inakemea na kulaani juu ya tukio hilo.

“Tumekusanyika hapa kwa ajili ya shughuli ya upatanishi ili kutengeneza umoja kutokana na tukio lililotokea la kushambuliwa kwa waandishi wa habari.

“Sisi Wamasai, tunalaani jambo lililotokea Agosti 15 mwaka huu la kushambuliwa na kujeruhiwa vibaya, kwa waandishi wa habari na mkalimani wao katika Kijiji cha Enduleni,”alisema Ngweshie.

Aidha, alisema kutokana na jambo hilo, wanafahamu kwamba litakuwa limeichukiza serikali na uongozi wa eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), hivyo kwa umoja wao wanaomba radhi juu ya tukio hilo.

“Kwa siku ya leo (jana), tumefanya mambo matatu; jambo la kwanza kuchinja ng’ombe watatu ikiwa ni ishara ya kumwaga damu, kuomba msamaha kwa NCAA.

“Ngo’mbe wa pili, ni ishara ya kuomba radhi kwa serikali, kwa tukio lililowatokea waandishi, na ngo’mbe wa tatu ni kwa ajili ya kumwomba radhi Rais Samia Suluhu Hassan.”

Akisoma tamko hilo la viongozi wa mila, Alaigwanani, Ndwala Ndoishie, alisema wakiwa kama viongozi wa mila, wao na jamii yao wako tayari kuhama na wanaunga mkono zoezi la uhamaji kwa hiari.

“Sisi Wamasai tunaoishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, tuko tayari kuhama na tunaunga mkono kazi ya uhamaji kwa hiari kutoka ndani ya hifadhi kwenda Msomera au sehemu nyingine tutakazochagua,”alisema Laigwanani huyo.

Vilevile, alisema kwa umoja wao, wametoa tamko hilo la utii kwa Rais Samia, kuhusu nia yake njema ya kuwataka wahame kwa hiari.

# Prof. Mbarawa awajia juu wahandisi washauri wapole

**Na Hamida Kamchalla,**
PANGANI

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema kuanzia sasa hataki kuona tena mhandisi mshauri ambaye hawezi kuwabana makandarasi wanaopewa zabuni za ujenzi wa miradi mikubwa nchini.

Amesema upole wa wahandisi ndiyo unaisababishia serikali hasara.

Aidha, Prof. Mbarawa, amewataka wahandisi hao kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu makandarasi wanaotekeleza miradi hiyo ili wanapofanya kinyume na mikataba yao wawabane na kuwapa adhabu inayostahili.

Alitoa maelekezo hayo jana alipotembelea na kukagua barabara ya Tungamaa/Mkwaja hadi Mkange, yenye urefu wa kilomita 95.2, ambayo imeigharimu zaidi ya Sh. bilioni 94.

Barabara hiyo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba, inatarajiwa kukamilika Machi, 31 mwaka 2025.

Akiwa katika ukaguzi huo, Waziri Mbarawa, alisema inapotokea mkandarasi amekwenda kinyume na utekelezaji au kuzembea, ni wajibu wa mhandisi mshauri kumpa onyo mara kwa mara ili aelewe makosa yake na inapotokea amepewa adhabu asione kama haikumstahili.

Vilevile, Prof. Mbarawa amekiri kuwa kwa sasa ujenzi wa mradi huo unasuasua.

“Mhandisi, wewe ndiye unasimamia mradi. Nataka kila kitu umuandikie, kwa sababu utakuwa umewaisaidia TANROADS (Wakala wa Barabara), wakati wa kutoa uamuzi.

“Sasa kama wewe mshauri mwelekezi hautaweka rekodi vizuri, wala hukumpa onyo, wakati wa kutoa uamuzi wa kumpa adhabu, tunataka ajue ni kwa nini amepewa adhabu hiyo.”alisema.

Awali, Meneja wa TANROADS, Mkoa wa Tanga, Eliazary Rweikiza, alisema mradi huo unatekelezwa na Kampuni ya Chona Railway 15 Bureau Group Corporation na unasimamiwa na Kampuni ya Beza Consulting Engineers PLC in JV with Cheil Engineering Co. Ltd.

Mkandarasi huyo, alitia saini mkataba wa kutekeleza mradi huo Agosti mwaka 2021 na kuanza kazi Aprili mwaka 2022.

Kwa mujibu wa Rweikiza, katika hatua za utekelezaji wa mradi, kumekuwa na matatizo mbalimbali ikiwemo kucheleweshwa uhamishwaji wa miundombinu ikiwemo mabomba ya majisafi, nguzo za umeme na nyaya za simu.



Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdallah (wa tatu kushoto), akifafanua jambo, wakati wa ziara ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (wa tano kushoto), ya kukagua ujenzi wa daraja la Mto Pangani jana. Wa nne kushoto ni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Naibu Waziri aagiza kila kabila kuanza kuonyesha utamaduni

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, ameagiza mikoa yote nchini kuanzisha matamasha ya kutangaza zao jipya la utalii wa kitamaduni, kwa kila kabila kuonyesha utamaduni wao ili kukuza utamaduni wa Kitanzania.

Akiwa jijini Arusha, Naibu Waziri, alisema serikali inatamani kuona kila mkoa unaanzisha utaratibu mahususi wa kufanya matamasha kama hayo.

Masanja alieleza matamanio hayo ya serikali, wakati wa hafla ya usiku wa utambulisho wa Tamasha la Maasai Festival, ambalo litafanyika kati ya Septemba 8 hadi 10 mwaka huu.

“Ninawapongeze sana wadau waliobuni tamasha hili kwa sababu jamii ya kifugaji ya kimasai, imekuwa kivutio kikubwa duniani, kutokana na kulinda utamaduni wao hasa kwenye mavazi na chakula.


“Rais Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa ya kuutangaza utalii wa nchi, kupitia filamu ya The Royal Tour, na matokeo yake yameonekana kupitia matokeo ya mafuriko ya watalii wanaokuja nchini.

...Hivyo, niombe mikoa yote hapa nchini kuunga mkono juhudi hizi, kwa kufanya matamasha ya kitamaduni, kwa lengo la kukuza zao jipya la utalii wa kimataduni na kutunza utamaduni wa makabila yetu.”

Naibu Waziri huyo, alisema serikali ipo tayari kushirikiana na wadau mbalimbali wanaonzisha utalii wa kimataduni katika kutangaza utalii na kuongeza mazao mapya ya utalii.

Mkurugenzi wa tamasha hilo, Lekoko Lepilali, alimweleza Naibu Waziri huyo kwamba, usiku wa mitindo ya mavazi ya kimasai, ni sehemu tu ya utambulisho wa Maasai Festival.

Alifafanua zaidi kuwa maonyesho hayo yatafanyika kwa siku tatu katika Mkoa wa Arusha, kwenye viwanja vya Ngarenaro.



# Upatikanaji petroli, dizeli wazidi kuwa shubiri Maswa

**Na Alex Sayi,** MASWA

UHABA wa mafuta ya petroli na dizeli katika Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu umezidi kuwa mbaya hali inayowaathiri wafanyabiashara wa nishati hizo pamoja na wateja.

Wakizungumza na Nipashe, wafanyabiashara wa nishati hiyo pamoja na wateja walieleza kuwa uhaba huo umekuwa kero kwao, kushusha hali ya kiuchumi katika shughuli zao.

Msimamizi wa moja ya kampuni ya kuuza mafuta wilayani hapa, Benjamini John alisema hali ya upatikanaji wa dola nchini imekuwa chanzo cha uhaba wa mafuta hayo.

Alieleza kuwa hali hiyo inawalazimu wauzaji hao wa jumla wa mafuta kuchelewa kuyauza mafuta yao wakihofia mabadiliko ya Dola nchini hali inayoweza kuwasababishia hasara.

"Wamepunguza kasi ya uuzaji wa mafuta kwa bei elekezi ya serikali kwa madai kuwa unaweza kuuza kwa bei ya chini halafu mwezi unaofuata ukakuta bei iko juu, hivyo ukashindwa kuyanunua mafuta kwa kuwa mtaji umekata," alisema John.

John aliongeza kuwa wao kama wauzaji wa rejareja wanalazimika kulichukua hilo wazo kutoka kwa wauzaji wa jumla, huku akibainisha kuwa mafuta nchini yapo kwa mujibu wa wauzaji hao wa jumla.

"Hali hii inaelekea miezi minne sasa, mfano kwa sasa tunaagiza gari mbili hadi tatu za mafuta lakini linakuja gari moja tu na vituo vingine havipati kabisa unakuta mafuta hakuna kutokana na sababu hiyo," alieleza John.

Mwenyekiti wa waendesha pikipiki 'Bodaboda' wilayani hapa, Emmanuel Makaranga, alisema kuwa uhaba wa mafuta na mabadiliko ya bei ya mafuta limekuwa tatizo kubwa katika shughuli zao kutokana na baadhi ya bodaboda wanalazimika kuacha kazi hiyo.

"Hali ya marejesho kwa wamiliki wa pikipiki imekuwa tatizo, mafuta hayapatikani, bei nazo zinabadilika kila wakati, tukiongeza bei wateja hawatuelewi wanatuona kama sisi ni matapeli," alisema Makaranga.

Dreva wa Bajaji, Shafii Mwendo alieleza kuwa uhaba wa mafuta umeendelea kuathiri shughuli zao huku wakilazimika kubeba abiria zaidi ya uwezo wa chombo ili kuokoa gharama za mafuta na changamoto ya uhaba.

"Kwa sisi tulioko vijijini mafuta tunayapata kwa wachuuzi lita moja tunanunua kwa Sh.4,000 mpaka Sh.4,500 ambayo hata kwa wamiliki wa kawaida wa vyombo vya usafiri ni ngumu kuimudu, hii inatusababishia hasara katika shughuli zetu za kila siku hususani katika kilimo cha umwagiliaji," alisema Jilaa Jagadi ambaye ni mkulima.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeelekeza upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa Mkoa wa Simiyu kuwa ni kati ya Sh.3,346 hadi Sh.3,358 bei ya kuanzia Agosti 2 mwaka huu.

## Hukumu ya kifo yaibua utata watuhumiwa wakiachiwa

**Na Aneth Ntungo,** SAUT

HUKUMU ya kunyongwa iliyotolewa na Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza kwa watuhumiwa watatu kati ya watano katika kesi ya mauaji dhidi ya January Kasahuke yaliyotokea katika Msitu wa Samina mkoani Geita, Februari mwaka huu imeibua utata.

Utata huo umeibuka baada ya watuhumiwa wawili kuachiwa huru katika mazingira ya kutatanisha wakati wenzao watatu wakihukumiwa kunyongwa.

Waliohukumiwa kifo katika kesi hiyo ni Juma Bulaka, Juma Kasanana na Bahati John, hali iliyosababisha upande wa utetezi kukata rufani katika Mahakama ya Rufani Mwanza.

Akitoa maelezo ya rufani hiyo, Wakili Costantin Mutalemwa alisema kufuatia hukumu namba 585/2017 iliyowahusu waleta rufani hao watatu, kutokutenda haki kwa kuwahukumu watuhumiwa watatu, kisha wawili kuachiliwa huru imesababisha kuwasilisha maombi ya kubatilisha hukumu hiyo.

Aidha, alieleza kuwa walioachiwa huru katika kesi hiyo ni Julius Kataha na Mbaraka Said, hivyo kuomba mahakama hiyo kuwaachilia huru watuhumiwa wengine kama ilivyofanyika kwa wale wawili.

Naye Wakili Steven Kitale, alieleza Mahakama kuwa wakata rufani walikuwa na haki ya kupewa hati ya mashtaka wakati kesi inasikilizwa, lakini wakata rufani hao hawakupewa hati hiyo na pia PH imetaja washtakiwa wote watano lakini mpaka sasa waliopo hatiani ni watatu tu.

Baada ya kuwasikiliza mawakili hao, Wakili Mwandamizi wa Serikali, Kastusi Ndamugoba alisema wakata rufani waliathirika na maamuzi ya Mahakama na haki haikutendeka vizuri maana kuna mapungufu katika hukumu yao.

Kulingana na upungufu huo Wakili Ndamugoba aliiomba Mahakama hiyo kuchukua hatua ya kuichunguza hukumu hiyo.

Naye Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji Fednand Wambali, alisema kutokana na hoja hizo za pande mbili wakata rufani wataendelea kukaa jela hadi kesi yao itakapoitwa kwa ajili ya kutajwa mbele ya Mahakama.




Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (kulia), akikabidhi kombe na cheti kwa Ofisa Matekelezo wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Alberto Nyingo, baada ya mfuko huo kuibuka mshindi wa pili wa taasisi, wakala na taasisi za umma (kundi la sekta ya hifadhi ya jamii) katika maonyesho ya 18 ya Biashara ya Afrika Mashariki yanayoendelea viwanja vya Furahisha jijini Mwanza jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Wafanyakazi wa ndani walipwe mishahara mipya'

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAAJIRI nchini wametakiwa kufuata sheria na kanuni mpya zilizowekwa na serikali juu ya upandishwaji wa mishahara kwa wafanyakazi ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wa ndani ambao kima chao cha chini ni Sh.60,000.

Ombi hilo limetolewa jana na baadhi ya wafanyakazi pamoja na viongozi wa mtandao wa wafanyakazi wa ndani kutoka mikoa sita.

Mtandao huo upo mkoani Mwanza kwa ajili ya semina na mafunzo wezeshi kwa wafanyakazi hao, lengo likiwa ni kuwawezesha kujilinda kimwili na kiafya pamoja na kuwalinda watoto wa waajiri wao pindi wakiwa katika kipindi cha balehe.

Mratibu wa mradi wa uwezeshaji wa mambo mbalimbali kwa wafanyakazi wa ndani kutoka Shirika la Wote Sawa, Domitila Faustin, licha ya kuishukuru serikali kusikia kilio cha kupandisha kima cha chini cha mishahara kufikia Sh.60,000 alisema utaratibu huo bado haujaanza kutumiwa na waajiri wengi nchini.

Kadhalika, aliiomba serikali kuendelea kufanya utaratibu wa kuanza kutekeleza mkataba wa kimataifa namba 189 unaoelezea kazi zenye staha kwa wafanyakazi wa ndani.

Mwezeshaji wa masuala ya jinsia na afya ya uzazi salama katika semina hiyo, Fortunata Scander alisema licha ya wafanyakazi wa ndani kuwa sehemu kubwa ya malezi kwa watoto wa waajiri lakini wanakosa elimu ya uzazi kwa ajili ya kujistiri wao pamoja na watoto wanaowalea pindi waingiapo katika kipindi cha balehe.

"Katika kipindi cha balehe wadada wa kazi wanabadilika tabia kama ilivyo kwa watu wengine na kuonekana kama wana kiburi na siyo wasikivu kama waajiri wanatakiwa kutambua kipindi hiki na kuwapa msaada na siyo kuwakaripia," alisema Scander.

Mmoja wa wafanyakazi hao kutoka mkoani Mwanza, Neema Salvatori alisema katika mafunzo hayo wamekumbushwa namna ya kujilinda na kujikinga na vishawishi ikiwa ni pamoja na kuwalinda na kuwatunza watoto wa waajiri wao pindi wanapoingia katika balehe.




Ukurasa 12

**Uchaguzi mbunge Mbarali huo, NEC yapuliza kipenga**



Ukurasa 13

Kuingia kwenye siasa haikuwa rahisi ilinipasa kubwaga kazi yangu serikalini




Ukurasa 14

**Ndivyo kifo cha vigogo wa Wagner kitavyowarudi Putin, Lukashenko**

siasa

JUMATANO AGOSTI 30, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

KUPANUKA BRICS

# Ni kusaidiana wenye vikwazo kupumua, kuinua biashara

• Bado kitendawili namna ambavyo Afrika inavyoweza kunufaika

**Na Nimi Mweta**

NCHI zinazoendelea na chache zilizoendelea zinazofungamana katika kundi la BRICS zikihusisha mataifa ya Brazil, Russia, India, China, South Africa, zinapanua wigo na kuongeza wanachama wengine.

Viongozi wake wamekutana Afrika Kusini wiki iliyopita ikiwa ni kama mkutano pacha na ule G20 kundi la nchi 20 zilizoendelea kiuchumi duniani unaofanyika Septemba 9 na 10 nchini India.

Wanachama wa kudumu wa kundi la BRICS waliokuwa watano sasa wameongezeka na kufikia 11 na bado wapo waalikwa au watazamaji.

Rais Samia Suluhu Hassan, mathalani, amehudhuria mkutano huo licha ya kuwa Tanzania siyo taifa 'mfikiriwa' wa uanachama BRICS, lakini hakuna tatizo endapo inahitaji kushiriki mikutano katika ngazi tofauti.

Hata pia kufanya mazungumzo ya ana kwa ana na viongozi muhimu kama Rais Samia alivyopata nafasi ya kufanya majadiliano ya kinachojiri hivi sasa na Rais Xi Jinping wa China bila kuhitaji kufanya ziara nchini humo ni jambo lenye tija kwa Tanzania.

Moja ya fursa za adhimu za mikutano hiyo ni kuwezesha nchi tofauti duniani kuwekana sawa, kukamilisha jitihada za kibalozi zilizopo na mara nyingine kufikia makubaliano.

Kundi la BRICS kwa upande mmoja linaonekana kama nchi zinazoendelea au za kusini, ila sivyo. Kimsingi ni kama umoja wa kushindana na ubabe wa kundi la kujihami wa nchi za Magharibi (NATO), kidiplomasia.

Licha ya kuwa baadhi ya wanachama wake wana uhusiano wa karibu na nchi za magharibi, hasa India, bado kwa kiasi fulani wana uwezo wa kuunda umoja wa kukemea hili au lile.




Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye mazungumzo na baadhi ya washiriki wa mkutano wa BRICS, Afrika Kusini wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

Ni kuwa na sauti ya ziada kidiplomasia na siyo kile kinachoamuliwa na nchi za Magharibi, zenye sauti kubwa zaidi katika mashirika ya Umoja wa Mataifa na kwa jumla zinatoa mashinikizo kwa nchi nyingine kuendana na matakwa yao.

Tofauti kati ya kilichokuwepo wakati wa harakati za nchi za Kusini au South South Cooperation, au zisizofungamana na upande wowote ni kuwa hivi sasa mifumo ya kimataifa ya utandawazi imeshika kasi.

Hata China ambayo kwa miaka mingi ilikuwa ina mipango yake yenyewe ya ushirikiano na nchi nyingine duniani kwa njia ya moja kwa moja mkakati wa Ukanda na Barabara - Belt and Road, sasa haina tena matumaini ya mpango huo kufanikiwa.

Msingi wake ulikuwa ni matazamio kuwa kufanya biashara au uwekezaji kati ya nchi na nchi, kutakuwa na tija. Hivyo ilitazamia kujenga mahusiano na Afrika, Asia na hata Ulaya na kwingineko kwa biashara ya moja kwa moja iliyojengwa na taasisi za kitaifa.

Kwa upande mwingine, kuna mtetemeko kiasi fulani wa mafungamano au ushirikiano makubwa hasa Asia, ambako Umoja wa Nchi za Mashariki ya Asia (ASEAN) kwa miaka mingi inaongozwa na Marekani.

Katika mvutano wa uchumi na kuvurugika kwa minyororo ya ongezeko la thamani hasa katika vifaa vya kielektroniki, nchi hizo haziwezi kufungamana na Marekani dhidi ya China. Ugomvi wa Marekani na China ni wa kimkakati, wa kuzuiwa kwa kampuni za Marekani kununua hisa au kuzinunua kampuni za China inazotaka, ikitanguliza sababu za kiusalama.

Kama haitoshi, China imeendelea kugangamala na suala la Taiwan kuunganishwa na dola ya China, wakati Taiwan inajiendesha kama jamhuri huru tangu China ikamilishe Mapinduzi ya Kikomunisti mwaka 1949. Marekani ina maslahi makubwa ya kibiashara Taiwan, ambayo kimsingi ni kama jimbo la Marekani kama ilivyo Israel, yaani kukiweka mashakani kisiwa hiki ni kugusa 'mboni ya jicho' la Marekani, kwani viongozi wa Taiwan wanafika bungeni Marekani kama vile wako nyumbani.

Pia wanatembelewa na viongozi wakuu wa Marekani kwa msingi wa mshikamano wa kidemokrasia, kuwa yaliyotokea Hong Kong katu yasifike Taiwan.

Hata hivyo, China haiwezi kukaa kimya ikiona Marekani inaipokonya tonge mdomoni ambalo ni kisiwa cha Taiwan.

Ujio wa BRICS na kuongeza wanachama zaidi unaangaliwa kama ni njia ya kuunda umoja tofauti na nchi za Magharibi hasa kiuchumi, ila kila mmoja wao anahitaji soko la Marekani, na kwa upande mwingine Amerika inalihitaji soko la China ila anazuiliwa kununua kampuni za huko.

Hiyo inafanya Marekani iwe ni mahali China inamwaga bidhaa ila hairuhusu uzalishaji kutekwa na wawekezaji wa Marekani au nchi nyingine za Magharibi, halafu hatari iliyowekwa juu ya Taiwan kwa sera yake ya kuiunganisha Taiwan na China haikubaliki ikihofiwa kuleta hatari ya vita.

Hivyo inavuruga minyororo ya thamani kwa 'micro-chips' mfano za simu, kompyuta, kadi za benki na vifaa vya kudaka mionzi au data ya teknolojia za kielektroniki kuhifadhi taarifa zisizohesabika katika kifaa hicho kidogo.

Hulka za mambo ya nje za China na Urusi zinafanana na sasa wanaunda umoja na wengine ambao hawana mazingira kama hayo ila wana mambo yao, ambako labda hawataki kukosolewa na nchi za Magharibi, hivyo wanapata mshikamano na joto ndani ya BRICS.

Hata hivyo, kimsingi hawawezi kufanya lolote kwa pamoja kwani soko kubwa duniani ni Marekani, Ulaya ikiwa imezorota kiasi,

**INAENDELEA UK. 12**




Wagombea na wanachama wa vyama vya siasa wakiangalia fomu baada ya uteuzi wa wagombea kata ya Nala mkoani Dodoma. **PICHA: NEC**

# Uchaguzi mbunge Mbarali huo, NEC yapuliza kipenga

**Na Mroki Mroki**

WAPIGA kura wa jimbo la Mbarali mkoani Mbeya na wa kata sita za Tanzania Bara, wana siku 33 za kusikiliza na kuamua nani awe mwakilishi wao bungeni na kwenye vikao vya halmashauri.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetangaza Septemba 19, 2023 kuwa ni siku ya kuwapigia kura mbunge na madiwani katika uchaguzi mdogo wa jimbo la Mbarali na kata sita za mikoa kadhaa Tanzania Bara.

Julai mosi mwaka huu Francis Mtega, mbunge wa Mbarali CCM, alifariki katika ajali iliyohusisha bodaboda na trekita -power tiller. Tangazo hilo linatolewa mapema Agosti 5, mwaka huu na na Mkurugenzi wa Uchaguzi, Ramadhani Kailima, akitoa taarifa kwa umma ya kuwepo uchaguzi huo mdogo.

Aidha, mchakato unaanzia Agosti 13 hadi 19 ambao ni wakati wa wagombea kuchukua fomu za uteuzi na uteuzi ulifanyika Agosti 19 na kampeni za uchaguzi zilianza Jumapili Agosti 20 zikitarajiwa kuendelea hadi Septemba 18.

> "Vyama vya siasa na wagombea pamoja na wafuasi wao wanapaswa kuepuka kufanya siasa za fujo na za vitisho dhidi ya upande mwingine.

Wagombea 14 kutoka vyama vya siasa 14 vyenye usajili kamili walichukua fomu za uteuzi na kati yao 13 wameteuliwa kuwania kiti hicho cha ubunge Mbarali.

Wamebakia 13 kwa sababu mgombea wa Chama cha NRA hakurejesha fomu. Walioteuliwa na vyama vyao kwenye mabano ni Halima Magambo (AAFP), Oswald Mndeva (DP), Zavely Seleka (UDP), Exavery Mwataga (CCK), Mary Daudi (UPDP), Modestus Kilufi (ACT-Wazalendo).

Wengine ni Morris Nkongolo (TLP), Hashim Mdemu (ADC), Fatuma Ligania (NLD), Mwajuma Milambo (UMD), Bahati Ndingo (CCM), Husseni Lusewa (ADA-TADEA) na Bariki Mwanyalu (Demokrasia Makini).

Aidha, vyama 17 vimejitokeza kuchukua fomu kwa ajili ya kuwania nafasi za udiwani katika kata sita za Tanzania Bara ambapo jumla ya wagombea 45 wameteuliwa kuwania nafasi hizo.

Kata zinazofanya uchaguzi mdogo na mikoa yake kwenye mabano ni Nala (Dodoma), Mfaranyaki na Mtyangimbole (Ruvuma), Mwaniko (Mwanza), Old Moshi Magharibi na Marangu Kitowo (Kilimanjaro)

Wagombea 58 walioteuliwa na NEC ni wale waliopendekezwa na vyama vyao kugombea ubunge na udiwani ambapo pia walijaza na kuwasilisha fomu za uteuzi katika Ofisi za Uchaguzi katika jimbo na kata zinazohusika.

Aidha, wagombea ubunge waliwasilisha fomu za uteuzi katika ofisi za wasimamizi wa uchaguzi wa jimbo na wagombea udiwani kwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata.

Halikadhalika , fomu za uteuzi za wagombea wote ziliwasilishwa siku ya uteuzi kabla ya saa 10 jioni na wagombea hawa wote siku ya uteuzi walijaza na kusaini mbele ya msimamizi wa uchaguzi fomu ya maadili ya uchaguzi.

Walijaza fomu hizo kukiri kuheshimu na kuyazingatia maadili ya uchaguzi yaliyosainiwa na viongozi wa vyama vyao mwaka 2020 wakati wa uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani kwa Tanzania Bara.

Uwepo wa maadili ya uchaguzi unalenga hasa kuwa na uchaguzi huru, wa haki, uwazi na wa kuaminika. Na kwamba amani, ustawi wa nchi, usalama wa raia, uhuru wa vyama vya siasa na utii wa sheria , kanuni na taratibu za uchaguzi ndio msingi wa uchaguzi ulio huru, haki na wenye kuzingatia ushiriki wa makundi yote ya jamii katika uchaguzi.

Vyama vya siasa, serikali na NEC walikubaliana kuwajibika kuyatekeleza maadili hayo yanayotokana na kifungu cha 124A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura ya 343.

Viongozi hao kwa pamoja walisema "Tutafanya jitihada za wazi kuhakikisha maadili haya yanajulikana na kuheshimiwa na wagombea pamoja na wanachama wote wa vyama vya siasa".

Sheria, kanuni na miongozo yote iliyotumika katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 bado inatumika na kufuatwa na vyama vya siasa, Tume ya Taifa ya Uchagzi na serikali katika chaguzi hizi ndogo za udiwani.

Tayari kampeni za uchaguzi zimeanza tangu siku moja baada ya uteuzi na zitaendelea hadi siku moja kabla ya siku ya kupiga kura. Wakati wote wa kampeni wagombea wanatakiwa kuzingatia sheria, kanuni za uchaguzi, maadili ya uchaguzi na ratiba za kampeni.

Uzingatiaji wa sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na ratiba za kampeni utasaidia kuweka uwanja huru na waamani wa ufanyaji wa uchaguzi.

Vyama vya siasa na wagombea pamoja na wafuasi wao wanapaswa kuepuka kufanya siasa za fujo na za vitisho dhidi ya upande mwingine.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura ya 343, imepewa jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura nchi nzima, kuratibu na kusimamia taasisi au asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo.

Tume itatoa elimu kwa wananchi katika maeneo yote yanayofanya uchaguzi mdogo. Lakini pia zipo asasi tatu ambazo zimepewa kibali na NEC kutoa elimu hiyo kwa baadhi ya maeneo.

Elimu hiyo inayotolewa ni ile ya kumuwezesha mpiga kura kutambua sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi ikiwa ni pamoja na utaratibu mzima wa kufunguliwa na kufungwa kwa vituo vya kupigia kura.

Lakini, pia elimu hiyo itasaidia kutoa hamasa kwa wananchi kutumia haki yao ya kikatiba katika kujitokeza kupiga kura na kuchagua viongozi wanaowataka.

Ni muhimu wananchi katika maeneo yote yanayofanya uchaguzi mdogo wakajitokeza kwa wingi kusikiliza sera za vyama na wagombea kisha wachague viongozi wanaowaofaa kujaza nafasi zilizo wazi.

***Mwandishi ni Ofisa Habari Msaidizi Mwandamizi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.***

## Kupanuka BRICS ni kusaidiana wenye vikwazo kupumua, kuinua biashara

**INATOKA UK. 11**

India bado haikidhi mahitaji kwani wastani wa kipato ni mdogo dola 2,500 kwa mwaka takribani mara mbili ya Tanzania, na nusu ya Indonesia.

Wanachama wa BRICS kutumia sarafu mojawapo badala ya dola hakujafanikiwa kwani watu wanahifadhi fedha zao nchi za Magharibi ambako kuna uhuru wa mtu binafsi na usalama. Kuwapo sarafu nyingine ni mbadala wa kurahisisha baadhi ya manunuzi kwa sasa, na siyo sarafu za kufanyia shughuli kama mikopo ya kibenki na ununuzi wa hisa.

Swali linalojitokeza ni kuhusu Afrika, kama uhusiano wa karibu zaidi na BRICS una faida yoyote, ambako jibu ni labda.

Yako maeneo ambako kuelewana kidiplomasia bila kubadili lolote katika yale ya msingi inasaidia, kwa mfano Rais Joko Widodo, kufanya ziara ya siku mbili hapa nchini akiwa njiani kuhudhuria mkutano huo wa BRICS, au mazungumzo na Rais Xi Jinping.

Hata hivyo dunia inachotaka kwa Afrika, iwe ni BRICS au Umoja wa Ulaya, Marekani, China na Urusi ni kukamilisha itifaki ya Soko Huru la Afrika, kwani kama bara ina soko kubwa kiasi linalokua kwa kasi.

Mengine yanabaki palepale, dunia nzima inataka biashara na hakuna mfungamano wa BRICS kujengewa reli kwa mikopo ya miaka 30 au 40 kama zamani. BRICS ni kujuana zaidi, na hiyo pia ina faida, halafu inawapa 'kampani' wanaotengwa na nchi za Magharibi kama ilivyo Urusi sasa.

FATMA FEREJ

# Kuingia kwenye siasa haikuwa rahisi ilinipasa kubwaga kazi yangu serikalini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

FATMA Abdulhabib Ferej ni mwanamama aliyeacha kazi serikalini na kuingia katika siasa kwa kugombea nafasi ya uwakilishi jimbo la Malindi lakini hakupata nafasi hiyo. Licha ya kutoswa hakupoa aligombea tena mwaka 2000 kupitia chama cha CUF na kukwama pia.

Hakupoa wala kukata tamaa mwaka 2005 akajitosa katika kinyang'anyiro nafasi hiyo ya uwakilishi katika jimbo hilo na kuibuka kidedea licha ya kukwepa mikuki mingi , anasema mwanasiasa huyo aliyezaliwa 1961 visiwani Zanzibar.

Alianza na utumishi wa serikali katika Wizara ya Elimu na kitaaluma ni mwalimu wa masomo ya sayansi, akieleza kuwa alisoma katika shule za msingi na sekondari Unguja na baada ya hapo, alipata shahada ya kwanza ya ualimu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ya pili ya ukutubi aliipatia Uingereza, kadhalika amesoma kozi fupi zikiwamo za komputa nchini Malaysia na India.

Mama huyu wa watoto sita, anasimulia kuwa hakuwa na ndoto ya kuwa mwanasiasa wala kuwa kiongozi lakini alishawishiwa na kushikwa mkono kugombea nafasi hiyo na kinamama.

"Wale wanaosema adui wa mwanamke ni mwanamke, nakataa mimi mwanamke hajawahi kuwa adui yangu bali alikuwa ni msaada kwangu, maana alinishawishi kugombea nafasi ya uwakilishi tena ndiye niliyemrithi nafasi ya uwakilishi Malindi,"anasema.

Anamtaja Hinaya Foum, ambaye ni marehemu kuwa ndiye aliyemshawishi wakati huo akiwa mtumishi serikalini, alikubali na kuelekea kupoteza kibarua chake, akiwataja wanawake wengine ambao wamemjengea uwezo kiuongozi kuwa ni spika wa zamani,Anne Makinda na mwanasiasa mkongwe Anna Abdallah.

"Walitujengea uwezo kivitendo na nadharia tena walitukasanya wanawake kutoka vyama mbalimbali na kutufunza kujiamini, uwajibikaji na uongozi, "anasema Fatma na kuongeza kuwa alivutiwa na mwanasiasa maarufu visiwani Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad (marehemu) akiwa katika viriri akihutubia.

Aidha, anasema haikuwa kazi rahisi hadi kushawishika kuingia katika siasa baada ya kutishika na siasa za mwaka 1995 ambapo ilikuwa na machafuko na matukio mengi ambayo hayakupendeza.

Anasimulia kuwa licha ya changamoto hizo za kiuchaguzi lakini ilipofika mwaka 2000 alishawishika vya kutosha na ikamlazimu kujitosa katika siasa na kuamua kuacha kazi serikali kwa sababu kipindi hicho ilikuwa hairuhusiwi watumishi wa umma kuingia katika siasa.



Fatma Ferej akizungumza na wanawake wanasiasa wa vyama mbalimbali wanaotarajiwa kutiania katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, katika mkutano unaoandaliwa na Chama cha Wanahabari Wanawake TAMWA- Zanzibar. **PICHA: TAMWA**

> Walionishawishi kazi yao ikawa rahisi, nilijijengea ujasiri na nikachukua fomu ya kugombea uwakilishi jimbo la Malindi kupitia Chama cha Wananchi CUF wakati huo.

"Walionishawishi kazi yao ikawa rahisi, nilijijengea ujasiri na nikachukua fomu ya kugombea uwakilishi jimbo la Malindi kupitia Chama cha Wananchi CUF wakati huo,"anasema mwanamama huyo.

Aidha, anasema alipata mafunzo ya uongozi kupitia chama chake cha CUF wakati huo na mmoja ya wakufunzi anayemtaja ni Dk. Bashiru Ali, akiongeza kuwa ushirikiano ni muhimu sana kwenye siasa na kwamba wakati wake aliupata kutoka kwa viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa bila ya kujali itikadi zake.

Kadhalika, anasema uchaguzi alioshiriki wa mwaka 2000 ulikuwa na machafuko mengi hali ambayo iliwapeleka baadhi ya Wazanzibari kuwa wakimbizi na baada ya zahama hiyo ya uchaguzi, CUF na CCM vililazimika kuingia katika mazungumzo ya pamoja na kuundwa mwafaka wa pili 2002 ambapo aliteuliwa kuwa kamishna wa tume ya pamoja ya rais chini ya Rais Amani Abeid Karume.

Alifanya kazi katika tume hiyo kuanzia 2002 hadi 2005 na uchaguzi wa mwaka 2005 ulikuwa afadhali.

"Mwaka 2005 niligombea tena uwakilishi jimbo la Malindi na kuingia katika chombo cha maamuzi Baraza la Wawakilishi na Bunge la Jamuhuri ya Muungano kupitia nafasi za wabunge wa baraza hilo,"anasema.

Katika kipindi hicho akiwa katika BWW wanawake wanaotoka majimboni walikuwa wachache mno na wengi walitoka katika viti maalumu, akisema mwaka 2010 hakugombea nafasi yoyote katika siasa lakini aliteuliwa kuwa mwakilishi wa kuteuliwa uliompa uteuzi wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, akitumikia nafasi hiyo mpaka mwaka 2015 bila kugombea tena uongozi jimboni, akiwaachia vijana.

Akizungumzia siasa baada ya kujiunga na ACT Wazalendo, anasema amekuwa mmoja ya wajumbe wa kikosi kazi cha kukusanya na kuratibu maoni ya marekebisho ya katiba, alichokiunda Rais Samia Suluhu Hassan.

**USHAURI ANAOBEBA**

Anasema ili kuwawezesha wanawake kugombea uongozi wa kisiasa ni lazima kuwe na uchaguzi huru na salama kwa sababu wengi wanakwamishwa kwa kuogopa zahama za uchaguzi mkuu.

"Tunajitahidi kujenga mazingira Zanzibar kuwa na uchaguzi huru na salama kwa sababu wanawake wengi hawezi kukimbizwa na mitutu ya bunduki,"anaonya Fatma ambae ni mjumbe wa Kamati Kuu ya ACT -Wazalendo.

Anasema kilichomfikisha hapo ni kujitambua na kuwa na ajenda ya kusimamia jambo, kujua matarajio ya waliomchagua, kuwa na ushirikiano na wananchi na ushiriki katika shughuli za kijamii.

"Unapokuwa karibu na wananchi kwa shida na raha na wanawake wapo vizuri kuliko wanaume, kinamama wana uwezo wa kubaki majimboni kwa kipindi kirefu,"anasema

Anawaasa wanawake viongozi wasiwe wanaficha uwezo wao, wawaeleze uhalisia wapiga kura kipato wanachokipata na kama watayafanya hayo wana nafasi ya kuendelea kubaki katika nafasi za uongozi majimboni.

Anasema kinamama wana nafasi nzuri ya kuendelea kubaki wanapopata nafasi za uongozi majimboni ikilinganishwa na wanaume kwa sababu wapo karibu zaidi na wananchi katika huduma za kijamii.

Anawataka viongozi wanawake na wanaotaka kuingia katika uongozi kusoma na kujua mambo mbalimbali ili inapowasilishwa bajeti kuu ya serikali kuwe na uwezo wa kutoa maoni yao katika kuchambua na kuchagia bajeti ya taifa.

"Wapo wawakilishi na wabunge tangu walipoingia katika vyombo hivyo hawajazungumza wala kuuliza maswali hivyo lazima wanawake mkubali kujifunza kila wakati na kukubali kufanya kazi kwa pamoja bila kujali itikadi za kisiasa ili kujadili masuala ya wanawake na kuyapatia ufumbuzi."

Fatma anawapa mbinu wanawake wanaotaka kugombea nafasi za uongozi, kuacha woga na kujiamini na kutojilemaza kuwaachia wanaume nafasi zote majimboni na kuongeza, "Tukiingia katika majimbo wanaume wanatuogopa, hivyo msihofu mjiamini maana uwezo tunao."

Anawasihi kujiheshimu kwa sababu kuwa viongozi isiwe kigezo cha kudharau watu na familia zao hivyo ni vyema kuheshimu na kuthamini watu.

Mwaka 2013 Fatma alitunukiwa Tunzo ya Mwanamke Jasiri na Ubalozi wa Marekani jijini Dar es Salaam, kutokana na kuwa mchapakazi wa kweli na jasiri katika kutekeleza majukumu yake.

Aidha, ni kutokana na mchango wake wa kuwaunganisha wanawake na kuwashawishi kukubali kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar (SUK) inayowahusisha CUF na CCM na leo imewaleta pamoja CCM na ACT-Wazalendo.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Ndivyo kifo cha vigogo wa Wagner kitavyowarudi Putin, Lukashenko

**Na Mwandishi Wetu**

KIFO cha viongozi na waasisi wa Wagner Group Yevgeny Prigozhin na naibu wake Dmitry Utkin, , wanaohofiwa kuuliwa na dola, kinadaiwa kuwa kinaweza kuwageuka Rais wa Urusi Vladimir Putin na mshirika pekee barani Ulaya Alexander Lukashenko wa Belarusi.

Baadhi ya wapenzi wa kiongozi huyo wakiandika kwenye machapisho mitandaoni wanawataja waliohusika na kifo hicho kama "wasaliti" wa Urusi.

Katika ujumbe mmoja kwenye video , kundi la mamluki hao liliendelea kusema: "Kuna mazungumzo mengi hivi sasa kuhusu kile ambacho kikundi cha Wagner kitafanya. Tunaweza kuwaambia jambo moja, "Tunaanza, jiandae kwa ajili yetu."

Kuna madai kuwa pamoja na hayo machafuko yaliyoachwa nyuma na mkuu wa Wagner Group Yevgeny Prigozhin, wakati alipoandaa uasi dhidi ya Urusi na serikali ya Putin, yamefungua "dirisha" kwa wafuasi wanaompinga Rais wa Belarus Alexander Lukashenko, wakilenga kudhoofisha msimamo wake.

Habari zinasema kifo cha Yevgeny Prigozhin kinaweza hatimaye kumgeuka pekee barani Ulaya Lukashenko, wataalam wameonya.

Prigozhin alikufa pamoja na mwandani na mtu wa muhimu kwake wa karibu Dmitry Utkin, baada ya ndege yao kuanguka uwanjani muda mfupi baada ya kuondoka Moscow Jumatano iliyopita. Kifo cha mkuu au chifu huyo wa Wagner kimeombolezwa kote duniani na katika kundi la mamluki wake na kumezuka uvumi kuhusu ni nini mustakabali wa genge hilo.

Mparaganyiko unaripotiwa kwamba kundi kubwa la mamluki hao walilazimishwa kupata hifadhi nchini Belarus baada ya jaribio la uasi mwezi Juni dhidi ya serikali ya Putin, ingawa kuna ripoti zinazoibuka kuwa Rais Alexander Lukashenko, amewaamuru waondoke baada ya Kremlin au serikali ya Urusi kushindwa kulipia makazi yao.

Viongozi wakuu wa upinzani nchini Belarus sasa wanatazama kwa karibu kuona jinsi hali hiyo itakavyotokea kwa matumaini ya kutumia mwanya wa kumsambaratisha Lukashenko kwa madai ya kutokuwa na uhakika au imani naye ili kumyumbisha mshirika huyo wa karibu wa Putin.

Awali wachambuzi waligusia kuwa huenda Putin atajaribu kuwajumuisha mamluki wa Wagner katika Jeshi la Urusi, au kulifuta shirika hilo, hata hivyo jana anaripotiwa kuanza kuwalazimisha askari hao kufanyakazi chini ya amri zake.

Kuwepo kwa Wagner huko Belarusi kulikuwa nguzo ya udhibiti wa Urusi dhidi ya nchi hiyo na tishio kubwa kwa uhuru wao lakini pia kwa majirani zake.

Upinzani wa Lukashenko unawasiliana na mashushu wao wakiratibu na Serikali ya Ukraine kujadili athari za kifo cha Prigozhin kwa mustakabali wa nchi yake.

Ingawa mapinduzi yake ya kijeshi hayakufaulu, lakini ushawishi wa Prigozhin kwa Warusi ulikuwa wazi na alikuwa amehama hivi karibuni kutoka katika makazi salama huko Belarus na kuanza kuvinjari kwenye jiji la Moscow.




Maombolezo ya Mkuu wa Wagner, Yevgeny Prigozhin (kushoto) Naibu Dimtry Utkin. **PICHA ZOTE: POLITICO**

> Anaweka wazi kwa kila mtu ndani ya Urusi na nje hatakabiliana na changamoto yoyote. Kuna uwezekano finyu kwamba Prigozhin hajafa, na hakuwepo kwenye ndege hiyo na ataonekana hivi karibuni.



Marais Vladimir Putin (kulia) na Alexander Lukashenko wa Belarusi.

**MUSTAKABALA WAGNER**

Wakati huo huo, kuna madai kuwa mamluki wa Wagner walikuwa wameanda na wana utaratibu wa utekelezaji ulioidhinishwa kwa muda mrefu katika kukabili tukio la kifo cha Yevgeny Prigozhin au Dmitry Utkin endapo vingetokea ambayo sasa vimetimia.

Mamluki wa Kundi la Wagner wanapanga njama ya "uhamasishaji kabambe " kulipiza kisasi kifo cha viongozi wake Yevgeny Prigozhin na Dmitry Utkin, baada ya wawili hao kuuawa katika ajali ya ndege ya Urusi karibu na Moscow.

Kundi hilo, lililokuwa likiongozwa na Prigozhin, sasa litatekeleza "utaratibu ulioidhinishwa na kuandaliwa kwa muda mrefu iwapo kutatokea kifo cha Yevgeny Prigozhin au Dmitry Utkin".

Kwa mujibu wa gazeti la Kirusi la Readovka, katika tukio la kifo cha Prigozhin, Wagner "utaratibu wa uhamasishaji bila kujali ni nani alikuwa na hatia kwa kifo chake upo".

Hata hivyo, haijabainika jinsi kundi hilo sasa litakavyoitikia kifo cha kiongozi wake, lakini kupitia chaneli zake, ujumbe wa hasira ulitumwa baada ya kubainika kuwa ndege ya Prigozhin na wenzake ilitunguliwa karibu na mji mkuu wa Urusi.

Akizungumza kwenye kipindi cha Leo cha Radio 4 cha BBC, Sir John Sawyers, mkuu wa zamani wa Shirika la Ujasusi la Uingereza -MI6, anasema kuwa "dalili zote zinaonyesha" kwa Putin "kumtolea nje" Prigozhin ilikuwa ni kitendo cha lazima ili "kudhibiti tena udhibiti wake."

Anaendelea: "Anaweka wazi kwa kila mtu ndani ya Urusi na nje hatakabiliana na changamoto yoyote. Kuna uwezekano finyu kwamba Prigozhin hajafa, na hakuwepo kwenye ndege hiyo na ataonekana hivi karibuni."

Jasusi huyo wa zamani pia anasema imani yake ni kwamba ndege iliyokuwa imembeba Prigozhin, makamanda wake na abiria wengine walioangamia huenda iliangushwa na "kifaa kilichokuwa ndani ambacho kiliishusha ghafla chini". **MITANDAO**



**HABARI DODOMA**

## Bilioni 1.4/- kutumika kutibu macho wanafunzi 104,938

**Na Thobias Mwanakatwe,** DODOMA

SHIRIKA la Sightsavers linatarajia kutumia Sh.bilioni 1.425 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa 'Macho Yangu' katika Mkoa wa Dodoma.

Mradi huo pamoja na mambo mengine unalenga kufanya uchunguzi wa macho kwa wanafunzi 104,938.

Ofisa Fedha wa shirika hilo, Roselyn Makundi, alibainisha hayo jana kwenye hafla ya kutambulisha mradi huo kwa wataalamu wa afya wa Mkoa wa Dodoma.

Alisema mradi huo pia utatekelezwa katika mikoa ya Singida na Morogoro na gharama za mradi wote kwa mikoa yote mitatu ni Sh.bilioni 4.3.

Makundi alisema Mkoa wa Dodoma itakuwa ni mara ya kwanza kwa shirika hilo kuleta mradi huo utakaotekelezwa kwa miaka minne na mgawanyo wa gharama za mradi katika Sh.bilioni 4.3 ni kwamba Singida itapata asilimia 13, Dodoma asilimia 48 na Morogoro asilimia 11.

Naye Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini Sightsavers, Doris Chalambo, alisema lengo la mradi ni kushirikiana na serikali na wadau wengine katika kutoa huduma bora, endelevu na jumuishi katika wilaya tano za Mkoa wa Dodoma.

Alisema mradi huo pamoja na kwamba unalenga watu wote lakini kipaumbele zaidi katika utoaji huduma za macho kitakuwa kwa watoto, watu wenye ulemavu na wanawake na huduma zitakazotolewa ni upasuaji mtoto wa jicho kwa watu 15,000, kutoa miwani 15,000.

Chalambo alisema pia utatoa huduma ya uchunguzi wa macho kwa wanafunzi 104,938 shule 95 za Mkoa wa Dodoma na kuwataka viongozi kutoa taarifa ya mrejesho wa kazi zilizofanyika ili kusaidia kupata ufumbuzi matatizo yaliyojitokeza kwenye utoaji huduma.

Mkurugenzi Mkuu wa Sightsavers, Godwin Kabalika, alisema pamoja na kwamba ni mara ya kwanza kwa shirika hilo kufanya kazi na Mkoa wa Dodoma ana matumaini utafanya vizuri kama ilivyokuwa kwa Mkoa wa Singida na Morogoro kadri kutakavyokuwa na ushirikiano wa watendaji wote.

Daktari Bingwa wa Macho katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Dk. Japhet Boniface, alisema katika mkoa huo wananchi wengi wanatatizo la macho, kwamba licha ya jitihada zinazochukuliwa na serikali lakini bado kuna tatizo la ukosefu wa vifaa vya matibabu ya macho na wataalamu.

# CCM yaingilia tabia uporaji, unyang'anyi bidhaa machinga

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetakiwa kutatua kero za wafanyabiashara kwenye masoko badala ya kuwakimbiza na kuwanyang'anya bidhaa zao.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, Adam Kimbisa alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara wa Soko la Sabasaba jijini humo kwenye mkutano wa kutatua kero zao.

Alisema halmashauri hiyo inapaswa kuwa karibu na wafanyabiashara hao badala ya kuwa maadui na kuwanyang'anya bidhaa suala ambalo limekuwa likileta chuki miongoni mwao na Jiji. "Kwenye masoko ni sehemu ya biashara ya kujiinua kiuchumi na sio maeneo ya vurugu, hivyo mnatakiwa kuwasikiliza na kutatua kero zao siyo kukimbizana na kuwanyanyasa," alisema.

Aliwaonya viongozi wa masoko kuacha tabia ya kugawa maeneo kwa kuwaangalia wenye uwezo wa kibiashara akisema kwa kufanya hivyo watakuwa wanahesabika kuwa wanapokea rushwa.


"Nimepokea malalamiko yanayowahusu viongozi ndani ya masoko, wengi wenu mnatoa nafasi za kuweka meza kwa viashiria vya kutaka mpewe kitu kidogo, (rushwa) tabia hiyo ni wazi mtasababisha wasio kuwa na uwezo kuendelea kuwa maskini," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wafanyabiashara hao kutowachagua viongozi kwa kuwaangalia sura na wapenda rushwa badala ya utendaji wao kwa kuwa wakifanya hivyo watashindwa kufikia malengo yao ya kujiinua kiuchumi kupitia biashara zao.

Awali, wakizungumza kwenye mkutano huo, wafanyabiashara hao walibainisha kuwa wananyang'anywa bidhaa zao na migambo ya Jiji badala ya kuwapatia elimu.

Halima Mchomvu mfanyabiashara wa mboga alisema wao hawana ukaribu na watumishi wa Jiji kutokana na tabia yao ya kunyang'anywa bidhaa hali ambayo imewasababishia kuyumba kwa mitaji yao ya biashara.

Mwenyekiti wa soko hilo, Athuman Makore alisema wafanyabiashara hao wamekuwa wakikabiliana na kero nyingi hali inayowasababishia kufanya biashara maeneo yasiyoruhusiwa.



Wabunge wakiimba wimbo wa Taifa katika kikao cha kwanza cha Bunge la 12 jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yaanza ukaguzi, kusajili upya viuatilifu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu imeanza kupitia upya usajili na viuatilifu vyote ili kuvibakisha vinavyofaa sokoni kulingana na aina ya zao, eneo na magonjwa yaliyopo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini kutakuwa na kiuatilifu kimoja cha magonjwa kwenye korosho.

Akijibu swali hilo, Mavunde alisema katika korosho kuna magonjwa makuu manne ambayo ni ubwiriunga, blaiti, chule na debeki yanayodhibitiwa kwa viuatilifu vyenye viambata amilifu tofauti.

"Ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa visumbufu vya mazao serikali itaendelea kuimarisha utafiti na kushauri wakulima kutumia viuatilifu vyenye tija zaidi katika kilimo," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema kumekuwapo na utitiri wa viuatilifu kwenye zao hilo na kuhoji serikali haioni umuhimu wa kutoa elimu kwa wakulima wakati wa kugawa viuatilifu hivyo.

"Naipongeza serikali kwa kusajili wakulima ili kutoa pembejeo na viuatilifu lakini kuna kundi kubwa la wakulima hadi sasa hawajasajiliwa Je? , serikali ina mpango gani wa kufanya usajili kwa wakulima hao," alihoji.

Mavunde akijibu maswali hayo, alisema utiriri wa viuatilifu unatokana na magonjwa ya mazao na wadudu waharibifu na kwamba kupitia Kituo cha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Naliendele na Bodi ya Korosho wataendelea kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi ya viuatilifu hivyo.

Aidha, alikiri kuna wakulima bado hawajasajiliwa na nguvu imeongezwa kupitia bodi hiyo kuongeza idadi ya rasilimali watu ili kufanikisha kusajili wakulima na wapate viuatilifu kwa wakati.

## Mbunge ahoji kuchelewa ujenzi wa soko na stendi ya kisasa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Singida Kaskazini (CCM), Ighondo Ramadhan, amehoji serikali lini itajenga soko na stendi ya kisasa eneo la Njiapanda Merya Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

Akijibu swali hilo bungeni jana, Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Festo Dugange alisema serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida imeanza utekelezaji wa hatua za awali za ujenzi wa Stendi ya Njiapanda ya Merya.

Alisema katika mwaka wa fedha 2019/20 halmashauri ilitenga Sh.milioni 10 na kufanya upimaji wa eneo la stendi, kufanya usafi na kusawazisha eneo.

Aidha, alisema serikali inakamilisha kufanya tathmini ya gharama za ujenzi wa stendi hiyo na kuanza kutenga bajeti katika mwaka wa fedha 2024/25 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

Alisema, "halmashauri inaendelea na maandalizi ya andiko la mradi wa soko na litakapokamilika litawasilishwa serikalini kwa ajili ya uchambuzi na endapo litakidhi vigezo litatengewa bajeti na kuanza ujenzi".





# Madaktari bingwa Ujerumani kutoa matibabu ya macho kwa wafungwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADAKTARI bingwa wa macho kutoka Ujerumani ambao wamepiga kambi katika Hospitali ya Rufani ya Mbeya, wamefika katika Gereza Kuu la Ruanda lililopo jijini Mbeya kwa lengo la kuwafanyia uchunguzi na kuwatibu wafungwa.

Kambi ya madaktari hao imefanyika kwa uratibu wa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, kwa kushirikiana na uongozi wa hospitali hiyo ambapo zaidi ya watu 200 wanatarajiwa kufanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho.

Juzi, madaktari hao waliwatembelea wafungwa walioko kwenye gereza hilo la Ruanda na kuwafanyia uchunguzi wa matatizo ya macho ambapo waliobainika kuwa na tatizo la mtoto wa jicho walitakiwa kwenda kufanyiwa upasuaji.

Naibu Waziri Mahundi ambaye ni Mbunge wa Viti Maalumu wa Mkoa wa Mbeya, alisema aliamua wafungwa hao wachunguzwe ili na wao wanufaike na kambi ya madaktari hao.

Alisema wafungwa waliko magereza ni raia wa kawaida ambao wakimaliza vifungo vyao wanatakiwa kurudi kwenye jamii kwenda kuendelea na shughuli mbalimbali za uzalishaji na hivyo wanatakiwa wawe na afya njema.

Alisema kutokana na hali hiyo ndio maana alikubaliana na uongozi wa hospitali ya rufani ya Mkoa wa Mbeya kuwanufaisha pia wafungwa walioko kwenye gereza hilo.

"Tunachoamini sisi ni kwamba walioko huku ndani ni wenzetu ambao waliteleza kwenye jamii, wameletwa huku kwa lengo la kupata mafunzo ili baada ya hapo warejee kwenye jamii kuendelea na majukumu yao," alisema Mhandisi Mahundi.

Alisema katika gereza hilo wanakusudia kuwafanyia uchunguzi wafungwa 150 na kwamba watakaobainika kuwa na matatizo watatibiwa kwa kufanyiwa upasuaji kwa watakaobainika kuwa na mtoto wa jicho.

Alisema kambi hiyo ni maalumu kwa ajili ya upasuaji wa mtoto wa jicho na siyo matatizo mengine yakiwamo ya kupatiwa miwani na matatizo mengine ya macho.

Mganga Mfawidhi wa Gereza Kuu la Ruanda Mbeya, Mrakibu wa Magereza, Dk. Alex Buhinu, alisema wafungwa wa gereza hilo wamekuwa wakikabiliwa na matatizo ya macho ambayo yamekuwa yakiwalazimu kwenda kutibiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mbeya.

Alisema baada ya kupata taarifa ya ujio wa madaktari bingwa wa macho waliamua kuwaandaa wafungwa 150 ambao wamekuwa wakisumbuliwa na matatizo hayo ya macho mara kwa mara.

"Tunashukuru sana kwa kuletea wataalamu hawa maana tumekuwa tukilazimika kuwapatia rufani wafungwa kwenda kutibiwa hospitalini lakini kwa sasa wamekuja hapahapa," alisema Dk. Buhinu.

Naye Mrakibu wa Magereza, Sebastian Mganga, alishukuru uongozi wa Hospitali ya Rufani ya Mbeya na Naibu Waziri Mahundi kwa kuratibu matibabu hayo ya macho kwa wafungwa na mahabusu wa gereza hilo.

Alisema ujio wa madaktari hao kwenye gereza hilo ulisaidia wafungwa hao kujiona sehemu ya jamii na wanastahili kupata huduma kama raia wa kawaida.



Baadhi ya watuhumiwa 14 wa wizi wa fedha za serikali mkoani Mbeya wanaodaiwa kuiba zaidi ya Sh. milioni 450 wakishuka kwenye gari la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), baada ya kufikishwa katika Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## DC ashauri taasisi za fedha kutoa matibabu afya ya akili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI za kifedha zimeshauriwa kuandaa programu ya matibabu ya afya ya akili kwa watumishi ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma ambazo wanastahili.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa alitoa ushauri huo juzi alipozungumza na wafanyakazi wa Benki ya CRDB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambao walikuwa wanafanya mazoezi ya viungo kwa ajili ya kuimarisha afya zao.

Alisema baadhi ya watumishi wa taasisi hizo wamekuwa wakiharibu huduma kwa kuwajibu vibaya wateja jambo ambalo linaweza likawa linasababishwa na matatizo ya afya ya akili.

"Nawapongeza kwa kuanzisha hizi huduma za kuimarisha afya za watumishi, muda mrefu mmekuwa mkifanya kazi mkiwa mmekaa na wataalamu wanasema kukaa muda mrefu kunasababisha madhara kwa hiyo hili mlilofanya ni jema lakini ongezeeni na kipengele cha afya ya akili," alisema Malisa.

Alizitaka taasisi zingine za kifedha kuwa na utaratibu wa kuwaruhusu wafanyakazi wake kufanya mazoezi ya viungo ili kuimarisha afya zao.

Meneja wa CRDB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Jenipher Tondi, alisema benki hiyo katika ukanda huo ina matawi 22 na kwamba wafanyakazi walioshiriki kwenye mazoezi hayo walikuwa zaidi ya 200.

# Wenyeviti mitaa, vijiji watakiwa kudhibiti uchomaji moto mashamba

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WENYEVITI wa mitaa na vijiji mkoani Njombe, wametakiwa kusimamia sheria ndogo za kuzuia uchomaji moto wakati wa kuandaa mashamba ili kuepuka hasara zinazoweza kujitokeza moto ukiingia kwenye maeneo mengine.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Ukaguzi wa Usalama wa Moto Mkoa wa Njombe, Mkaguzi Hilary Kobero, alisema wanaendelea kutoa elimu kuhusiana na uandaaji wa mashamba bila ya kusababisha hasara.

"Miongoni mwa njia ambazo wanapaswa kuzifuata kweli kweli ni zile sheria ndogo ambazo zimewekwa katika mamlaka za serikali za vijiji, sheria ziko wazi zinasema muda, hali ya hewa ambayo inapaswa ifuatwe lakini na idadi ya watu wanaopaswa wawepo wakati wa kuwasha moto," alisema Mkaguzi Kobero.

Alisema kuwa "Mfano Kijiji cha Idunda wanasiku maalumu ya Jumatano kwa hiyo haupaswi kuandaa shamba kwa njia ya kuchoma moto bila kibali maalumu kutoka kwa Mwenyekiti wa Kitongoji lakini kuna siku maalumu wamejiwekea iwe Jumatano tu kwa kijiji kizima na vijiji vingine vinasiku yao," alisema.

Hata hivyo, alisema muda maalumu ambao mtu anatakiwa kuandaa mashamba hayo ni asubuhi au jioni lakini kwa kuzingatia hali ya hewa.

"Kwa mfano kama hali ya hewa ikiwa upepo mkali, siku hiyo kuna upepo mkali hata kama ni siku rasmi ya kuwasha moto lakini haipaswi kufanya hivyo kwa sababu hali ya hewa hairuhusu kufanya hivyo, kwa maana ya kwamba upepo ukiwa mkali ukichoma moto utaruka kwenda mahali pengine," alisema Kobero.

Aidha, alisisitiza kuwa wananchi wakiona hali ya hewa ya upepo hawapaswi kuchoma moto hata kama wamepewa kibali.

"Lakini idadi ya watu hairuhusiwi kuchoma moto kama idadi ya watu hawapo kwa hiyo, kuna idadi ya watu angalau wakiwa wanne au watano wawepo wakati wa kuchoma moto ili kuzuia moto usije ukaruka na mpaka unazima kabisa ndio mnaondoka," alisema.

Mkaguzi Kobero alitoa wito kuchongwa barabara za kutosha hasa kwenye mashamba ya miti ili kusaidia moto ukitoroka usiingie.

Alitoa rai kwa maofisa kilimo kutoa elimu kwa wakulima ya kutumia njia mbadala ya kuandaa mashamba na siyo kuchoma moto.

Kobero alisema una uzoefu unaonyesha mwaka jana kwa Wilaya ya Njombe walipata hasara kubwa kutokana na moto ambao umekuwa ukiunguza mali mbalimbali.

Mmoja wa wakazi wa Njombe, Samwel Mgaya, alitoa wito kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kujielekeza zaidi kutoa elimu maeneo ya vijijini.



# Tume ya Uchaguzi Zanzibar yapata Makamu Mwenyekiti

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SIKU moja baada ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kumwapisha Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), wajumbe sita wa tume hiyo wamemteua Jaji Aziza Iddi Suwed kuwa makamu mwenyekiti.

Jaji Aziza ni miongoni mwa wajumbe saba walioteuliwa na Rais na kuapishwa juzi wakiongozwa na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji George Joseph Kazi.

Uteuzi huo wa makamu mwenyekiti umefanyika kwa mujibu wa Ibara ya 119 (2) (b) ya Katiba ya Zanzibar ambacho kimeipa mamlaka Tume ya Uchaguzi katika kikao cha kwanza kuteua makamu mwenyekiti miongoni mwa wajumbe walioteuliwa na Rais.

Jaji Aziza alisema atahakikisha anafanya kazi kwa ushirikiano na watendaji wa tume hiyo ili kuitumikia nchi pamoja na wananchi wote.

Aidha, aliwataka wananchi na wanasiasa kuithamini tume hiyo na kusema kuwa itasimamia chaguzi zote kwa uhuru na haki.

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imefanya kikao chake cha kwanza katika ofisi za tume hiyo zilizopo Maisara mjini Zanzibar chini ya Mwenyekiti wake, Jaji George Joseph Kazi.

Akizungumza baada ya kuteuliwa Jaji George alisema ataiongoza tume kwa mujibu wa sheria na taratibu, hivyo atahakikisha utekelezaji mzuri katika kufuata misingi ya demokrasia na utawala bora.

# Sensa ya taasisi za kiuchumi kufanyika mwezi ujao

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI inatarajia kufanya sensa ya taasisi za kiuchumi Septemba mwaka huu katika mikoa yote ya Unguja na Pemba.

Madhumuni ya sensa hiyo ni kupatikana orodha kamili ya taasisi zote zenye kuzalisha na kutoa huduma za kiuchumi na kijamii.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Mazizini Nje ya Mji wa Zanzibar, Mratibu wa shughuli za kijamii na kiuchumi wa ofisi hiyo, Hamisa Suleiman Faki, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu sensa hiyo itakavyowezesha kupata idadi ya shughuli za kiuchumi na kijamii zilizopo katika sekta isiyo rasmi na rasmi.

Alisema pia itasaidia kupata sampuli kwa ajili ya tafiti za kiuchumi na kijamii zitakazofanyika baadaye na maeneo yatakayohusika na sensa hiyo ni shughuli za kiuchumi zinazoendeshwa ndani ya majengo au sehemu za wazi ambazo ni za kudumu.

"Kwa mantiki hii, uorodheshaji huu hautahusisha taasisi au shughuli isiyo na jengo na wala sehemu ya kudumu ya kuendesha shughuli zake mfano shughuli zinazofanyika katika maeneo ya wazi nje ya soko, biashara za mikononi maarufu machinga, masoko ya muda, madereva taksi wasio na vituo rasmi, shughuli za kilimo na uvuvi ambazo haziko chini ya vikundi, ushirika au jumuiya maalum," alisema.

Alizitaja baadhi ya sekta zitakazohusishwa katika uorodheshaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi ni pamoja na uchimbaji wa madini, kokoto, mchanga, uzalishaji wa bidhaa viwandani, usambazaji wa umeme, gesi na maji, maeneo ya ujenzi, utengenezaji magari, pikipiki, hoteli, migahawa na shughuli za biashara.

Aidha, alisema matokeo ya sensa hiyo yatatoa picha halisi ya idadi ya shughuli za kiuchumi na kijamii, taarifa hizo zitasaidia pia kujua ukubwa wa uchumi na kujua utendaji katika sekta hizo za kiuchumi.

Pia aliwahakikishia wananchi watakaohojiwa kuwa taarifa watakazotoa zitakuwa siri na hazitatolewa kwa mtu mwingine zaidi ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na zitatumika kwa ajili ya matumizi ya kitakwimu.

Hata hivyo alisema wadadisi watakaoshindwa kutunza siri wataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu Sura Namba 351 ikiwa ni kutozwa faini, kutumikia kifungo jela au vyote viwili kwa pamoja.

Hivyo, aliwataka wananchi watakaofikiwa na sensa hiyo, kushirikiana na wadadisi watakaofika katika maeneo yao kwa kuwapa taarifa sahihi kwa lengo la kupata takwimu sahihi za kupanga mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikata utepe kuashiria kupokea gari la kliniki lililotolewa na Amref Health Africa kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwenye maeneo yasiyofikika wakati wa hafla ya mbio za Uzazi na Maisha Wogging jijini Zanzibar hivi karibuni. Wengine ni Mke wa Rais, Mama Mariam Mwinyi (kulia), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Amref Health Africa, Githinji Hitahi (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Amref Tanzania, Dk. Florence Temu (katikati). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara ya Mambo ya Nje, SMZ zatakiwa kushirikiana

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameagiza kuwapo na ushirikiano wa karibu baina ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Serikali ya Mapindizi ya Zanzibar.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu Zanzibar, alipozungumza na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Zanzibar, Balozi Silima Kombo Haji, aliyefika kujitambulisha.

Rais Dk. Mwinyi alisema taasisi mbili hizo zinategemeana kwenye ushirikiano wa majukumu yao hasa kwenye masuala yanayohusu mambo ya kimataifa.

"Mara zote tumekuwa tukiihitaji ushirikiano na ofisi hii (Idara ya Mambo ya Nje, Zanzibar) hasa kwa mambo ya kimataifa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar milango yetu ipo wazi kutoa ushirikiano na ofisi yenu, kama kukiwa na changamoto yoyote usisite kutupa taarifa na tutaitatua kwa hatua kwa kukupa ushirikiano unaostahili ili utimize majukumu yako," alisema Dk. Mwinyi. Aidha, alimtaka Balozi Silima ambaye ni Balozi wa Tanzania nchini Sudani kuwa kiungo mzuri kwa serikali kwenye eneo la Ukanda wa Afrika Mashariki na Kimataifa.

Pia Rais Dk. Mwinyi alimpa pole balozi huyo kwa matatizo waliyoyapata Sudani wanakoiwakilisha Tanzania kimataifa kutokana na changamoto za vita zinazoendelea nchini humo.

Dk. Mwinyi, alitumia fursa hiyo kumkaribisha nyumbani kuendeleza majukumu yake ya ujenzi wa taifa na kuitakia amani nchi ya Sudan kwa kuiombea kurejea kwenye amani yao ya zamani.

Naye Balozi Silima alimwahidi Rais Dk. Mwinyi ushirikiano wenye tija katika utekelezaji wa majukumu yao ya kusimamia huduma za diplomasia na itifaki katika kukuza ushirikiano wa kimataifa na kikanda kwa nyanja zote za uchumi na siasa.

Balozi Silima alisema atatekeleza vema majukumu yake kwa uaminifu na juhudi kubwa kwa kutumia taaluma aliyonayo, uzoefu na juhudi zake kuyafanikisha.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
ONE STOP JUDICIAL CENTER OF TEMEKE
AT TEMEKE

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 255 OF 2022

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE DAVID JOHN GATRELL

FORM NO. 84

**NOTICE TO CREDITORS**
**Made under Rule 111 of the probate Rules, G.N No.369 of 1963**

**NOTICE** is hereby given that all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the above-named **DAVID JOHN GATRELL** deceased who died at the **United Kingdom on the 02nd day of August, 2021** and letters of administration was granted to me by the **High Court of United Republic of Tanzania One stop Judicial Center of Temeke at Temeke on the 16th June, 2023,** are hereby required to send in their claims to me at the following address within which I shall proceed to hand over the assets to the persons entitled thereto having regard only to the claims of which I shall then have had notice.

**JONATHAN BEDDOE TAYLOR,**
**Safe Waste Incinerator Company Limited,**
**Msasani Peninsula Chole Road, House No. 76,**
**P.O.Box 14111,**
**Kinondoni, Dar es salaam.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**FRANCIS MATHIAS FRANCIS** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index nambas. **3827/0081** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NYIHOGO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0139/0664** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MTWARA TECH. SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/4518/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAMSON GABBY MUNWE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIES** yenye usajili namba **T501 DBV** na CHASSIS NAMBA: **ACU100002034.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/5387/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **CHRISTOPHER SEIF KAPELA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 583 CQQ.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/MUL/RB/148550/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0753933206.**

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 95/ 2023

In the matter of the Estate of the late PAMELA EMANUEL MLINGI of AREA E within Dodoma Region

AND

IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY EMANUEL JANUARY MLINGI

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 30 Day of August,2023

**Date at Dodoma this 2nd Day of August, 2023**

COURT SEAL DODOMA

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE I/c DODOMA DISTRICT

IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE
AT KOROGWE

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO...25...OF 2023

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MAGRETH MSEKWA

AND

IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTATION BY AISHA OMAR KIGODA

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSON Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be field on or before the th day of the September 2023

**Date at Korogwe this 14th day of August 2023**

DISTRICT COURT KOROGWE TANZANIA

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE
RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE DISTRICT

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

AGNES WILIAM KADUDU Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba ya usajili MC 475 CYB,model namba LNQPCK ,rangi nyeuzi,namba ya kadi ni 8797029,jina la kwenye kadi ni WU ZHOU INVESTMENT COMPANY LIMITED,Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi PHQ/MOR/GAI/665/2023.

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**ALLEN FREDRICK DAFTARI** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba **TAE 139537** ilyotolewa **PCO DAR ES SALAAM** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/TAN/TAN/357/2023**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
WILAYA MOROGORO
LILILOPO MOROGORO
RUFAA NAMBA 19 YA 2023
HUSSEIN SHABANI MIZORA ............MRUFANI
DHIDI YA
MARIAM MARTIN............WAJIBU MAOMBI
WITO/KUITWA SHAURINI KWA

**MARIAM MARTIN**
Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 31/8/2023 mbele ya Mwenyekiti M. Khasim wewe mwenyewe binafsi au mtume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hutahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi
.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 7 mwezi Agosti 2023

**FM. KHASIM**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MOROGORO.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA MVOMERO
ILIYOPO MVOMERO
KESI YA MADAI NAMBA 23 YA 2023
KATI YA
TATU HATIBU RAJABU..................CLAIMANT
NA
KUBILU PAULO.....................RESPONDENT

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

UNAJULISHWA KUBILU PAULO MDAIWA KWENYE KESI HII KUWA KESI YAKO ITATAJWA TENA TAREHE 31/08/2023.MAHAKAMA YA WILAYA MVOMERO,HIVYO KWA TAARIFA HII UNAJULISHWA KUJA MAHAKAMANI KWA AJILI YA KULETA UTETEZI WAKO NA KAMA UTASHINDWA BASI KESI HII ITAPANGWA KUSIKILIZWA UPANDE MMOJA BILA UWEPO WAKO.

HAKIMU

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
LA WILAYA DODOMA LILILOKO DODOMA

MAOMBI MADOGO NA 238 YA MWAKA 2023

ELIZABETH SEMFUKWE...........................MDAI

VERSUS

DAVID MGONGO..................................MDAIWA

KWA
DAVID MGONGO

**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa Kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Makala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Dodoma wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 01.09.2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** - Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi Yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/ Muhuri wa Baraza hili Leo tarehe 18 ya Mwezi wa AGOSTI, 2023.

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA TANZANIA

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,
WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA/ KIMATAIFA

## Uganda yamshtaki raia wake madai kuvunja sheria ushoga

**KAMPALA,** Uganda

WAENDESHA mashtaka nchini Uganda wamesema kuwa kijana mwenye umri wa miaka 20 amefunguliwa mashtaka kwa madai ya kujihusisha na mahusiano ya mapenzi ya jinsia moja, ambayo yanapingwa vikali nchini humo.

Uganda mwezi Mei mwaka huu, ilipitisha mojawapo ya sheria kali zaidi duniani inayolenga jumuiya ya watu wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja (LGBT) na kwamba kijana huyo amekuwa raia wa kwanza kushtakiwa kutokana na kuvunja sheria hiyo ambayo inapendekeza hadi adhabu ya kifo.

Pia ilielezwa kuwa sheria hiyo inaagiza kifungo cha maisha jela na kifo endapo kosa la kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja litajirudi kwa mtuhumiwa, kwa kuhusisha mtoto mdogo, mzee au mtu mwenye ulemavu.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka iliyoonekana na shirika la habari la Reuters, mshtakiwa alishtakiwa Agosti 18, mwaka huu kwa ulawiti uliokithiri baada ya kufanya ngono kinyume cha sheria na mwanamume mwenye umri wa miaka 41.

Msemaji wa ofisi ya mkurugenzi wa mashtaka ya umma, Jacqueline Okui, alisema "Kwa kuwa ni kosa la kifo linalosikilizwa na Mahakama Kuu, alisomewa shtaka hilo na kuelezwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi na kurudishwa rumande."

Ilielezwa kuwa Okui, hakutoa maelezo ya ziada kuhusu kesi hiyo, licha ya kueleza kuwa hakuwa na habari nyingine kuhusu mtu mwingine yeyote ambaye alishtakiwa kwa makosa hayo, kabla ya shtaka hilo.

Justine Balya, wakili wa mshtakiwa, alisema anaamini sheria yote ni kinyume cha katiba, akidai kuwa ilipingwa mahakamani, lakini majaji bado hawajashughulikia kesi hiyo.

Aidha, Balya alidai kuwa watu wengine wanne wamefunguliwa mashtaka chini ya sheria hiyo tangu ilipotungwa na kwamba mteja wake alikuwa wa kwanza kushtakiwa kwa kosa la kulawiti, huku akikataa kutoa maoni juu ya maelezo ya kesi yake.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa serikali za mataifa ya Magharibi na mashirika ya haki za binadamu yamekuwa yakiipinga vikali sheria hiyo dhidi ya wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja, huku Uganda ikiendelea kubaki na msimamo wake, kuwa haikotayari kuona tamaduni na maadili ya taifa hilo yakivunjwa. **BBC**



Nabii Lillian Mock kutoka Marekani, akizungumza wakati wa kongamano lililoandaliwa na vijana wa Kanisa la Dorcus Christian Ministries la Manabii na Mitume jijini Dar es Salaam jana kwa ajili ya kuliombea taifa pamoja na vijana kutokana na mmomonyoka wa maadili. Kushoto ni Mwenyekiti wa Idara ya vijana wa kanisa hilo, Godfrey Fungo na Nabii Lisa Ellioh kutoka Marekani. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# 'Tulikagua nyumba ya mke wa Msuya hadi usiku wa manane'

**Na Grace Gurisha**

MKUU wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, SSP David Mwanahe (56), amedai mahakamani kuwa walifanya upekuzi katika nyumba ya aliyekuwa mke wa Erasto Msuya 'Bilionea Msuya', Miriam Mrita hadi saa nane usiku kutokana na nyumba hiyo kuwa kubwa na walihitaji kukamilisha kazi waliyopewa.

Vilevile, amedai upekuzi huo ulikuwa na lengo la kupata vielelezo ambavyo vitawasaidia katika kesi ya mauaji ya mdogo wa marehemu Bilionea Msuya, Aneth Msuya. Walipata suti ya kike, mikufu inayodhaniwa kuwa ni ya dhahabu na kadi mbalimbali za magari.

SSP Mwanahe alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi wake kama mpelelezi wa kesi hiyo aliyetoka katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) kwa ajili ya kuongeza nguvu kwa maelekezo ya aliyekuwa DCI, Kamishna Diwani Athuman.

Alidai kuwa baada ya kusikiliza maelezo ya Getrude (dada wa kazi wa Aneth), yeye kama mpelelezi alibaini kuwa binti huyo hastahili kuwa mshtakiwa, bali anastahili kuwa shahidi wa kesi hiyo na alitoa maelekezo kwa askari wa kike Esther aandike maelezo kama shahidi.

Baada ya hapo, shahidi huyo alidai kuwa alitoa taarifa kwa RCO Temeke, SSP Mchovu na pia alimjulisha bosi wake, Kamishna Athuman kwa yale yote yaliyojitokeza na hatua waliyofikia.

"Hapo sasa tukaanza ufuatiliaji wa kuanza safari ya kwenda mkoani Arusha kufanya upelelezi, baada ya kupata taarifa kutoka kwa mhusika. Tuliondoka Dar es Salaam Agosti 4, 2016 kati ya saa tano na nusu na saa sita usiku. Tulifika alfajiri ya Agosti 5, 2016.

"Mimi kama kiongozi, nilimtaarifa Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kipolisi Arusha, SSP George Katabazi kumjulisha kwamba tuko Arusha kwa ajili ya upelelezi. Aliridhia na akatueleza kama tutahitaji msaada wowote tumjulishe," alidai SSP Mwanahe.

Alidai wakati wanaendelea na upelelezi kwa taarifa za kintelejinsia na za kutoka kwa wasiri, walipata taarifa kuwa mhusika wanayemtafuta yuko maeneo ya Klabu ya Tembo na walifanikiwa kumpata huko.

Shahidi huyo alidai alijitambulisha kwake na mtuhumiwa akajitambulisha kuwa anaitwa Miriam Mrita. Baada ya kutambuana, alimtaka kwenda naye hadi ofisi ya RCO Arusha ili apate kitabu cha ukaguzi, walitoka eneo hilo hadi Makao Makuu ya Polisi Arusha.

Alidai walipofika ofisini kwa RCO majira ya saa mbili usiku, hawakumpata kwa kuwa alikuwa amekwenda kushughulikia tukio, hivyo alimpigia simu akaomba wamsubiri. Alifika saa nne na nusu usiku.

"Nilimpa maelezo mafupi na kumweleza kwamba tumempata mtuhumiwa na tunataka kwenda kufanya upekuzi nyumbani kwake. Afande aliridhia na kunikabidhi kitabu cha ukaguzi na kumwahidi kumpa mrejesho kitakachojiri.

"Nilimtaka mtuhumiwa atuongoze nyumbani kwake anapoishi ili tukafanye upekuzi, alituongoza hadi eneo la Sakina kwa Idd. Huko nilimtafuta mjumbe ambaye ni shahidi huru Jacob Sabore, nikamweleza dhumuni la kwenda huko. Alitaka nioneshe vitambulisho vya polisi na nyaraka ya upekuzi," alidai.

Alidai kuwa kwa sababu muda ulikuwa umekwenda sana - ilikuwa ni saa sita usiku, walifanya upekuzi hadi saa 8:41 usiku kwa sababu nyumba ilikuwa kubwa. Alifanikiwa kupata suti ya kike, mikufu inayodhaniwa kuwa ni ya dhahabu na kadi mbalimbali za magari pamoja na simu tatu.

Baada ya kuvipata hivyo vitu, aliviorodhesha kwenye kitabu cha upekuzi. Mtuhumiwa, shahidi huru na yeye walitia saini nyaraka hizo. Pia walimtaka awaoneshe magari hayo kiuhalisia, aliwaeleza kuwa magari hayo yako kwenye hoteli yake ya SG.

"Wakati tunatoka huko nilimpigia simu SSP Katabazi na kumweleza kuwa tunaelekea kwenye hoteli ya SG na yeye alitueleza kuwa tutakutana naye huko. Tulikutana na kuona magari hayo ispokuwa gari moja, ambapo Katabazi aliniambia kuwa masuala ya magari nimwachie yeye," alidai.

Shahidi huyo alidai kuwa Agosti 6, 2016, walianza safari ya kurudi Dar es Salaam, walifika Korogwe saa nane na nusu alasiri. Alitoa muda wa kupumzika kwa sababu dereva alikuwa hajapumzika, Vigwaza walifika saa 12 jioni hadi kufika Chang'ombe Polisi ilikuwa saa tatu usiku.

"Kwa muda huo tuliofika, tulitaka mtuhumiwa Miriam apumzike na apate chakula na pia askari wangu na wao walikuwa wamechoka. Kwa hiyo, nilitaka wapumzike. Nilitoa taarifa kwa RCO Mchovu kuwa mtuhumiwa hajahojiwa," alidai.

SSP Mwanahe alidai kuwa anachofahamu Agosti 7, 2016, baada ya Afande Mchovu kumteua Koplo Mwajuma amhoji na kuandika maelezo ya onyo, alipata taarifa kuwa Mrita amekiri kuhusika katika tukio la mauaji ya Aneth Msuya na alitoa Sh. milioni 20 ili mauaji yatekelezwe.

Pia, tarehe hiyo Mrita alifanyiwa gwaride la utambuzi, Getrude Mfuru alimtambua. Kwa sababu alikiri polisi, walipeleka kwa mlinzi wa amani katika Mahakama ya Mwanzo Ilala mbele ya Mheshimiwa Leonia Kagumuro ambako alitoa maelezo yake ya hungamo.

Kutokana na taarifa walizozipata kutoka kwa Mrita, alipiga simu kwa viongozi wake, baada ya kumtaja Ray, kwa hiyo simu ilipigwa Makao Makuu ya Polisi Arusha kwa ajili ya kumpata mtuhumiwa mwingine.

Alidai kuwa alipewa taarifa kuwa Agosti 19, 2016, Ray alikamatwa. Alipewa jukumu tena kwenda kumchukua mtuhumiwa huyo ili amlete Dar es Salaam.

Alidai kuwa siku hiyohiyo, walisafiri kurudi Dar es Salaam wakiwa na mtuhumiwa pamoja na vielelezo. Walipofika mtuhumiwa alifanyiwa gwaride la utambuzi na alitambuliwa na Mfuru Agosti 21, 2016. Kesi hiyo itaendelea leo kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa mashtaka.

Katika kesi hiyo, Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji hayo ya wifi yake, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam, amekiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo. Mshtakiwa mwingine ni Revocatus Muyela.

# KLABU DARAJA LA KWANZA Z'BAR ZAIANGUKIA ZFF KUSHUKA TIMU 8

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKATIBU wa klabu za Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja wameliomba Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kupitia bodi ya ligi kuangalia upya kanuni ya kushuka daraja timu nane msimu huu katika ligi hiyo yenye timu 20.

**Ligi hiyo kwa msimu huu itachezwa kwa mfumo wa makundi mawili kila moja likiwa na timu 10 ambapo kila kundi zitashuka timu nne zilizomaliza nafasi ya chini.**

Kwa mujibu wa kanuni ya kuendesha mashindano ya msimu huu wa 2023/24 sura ya nne kifungu cha (2), kinaeleza jumla ya timu nane zitashuka daraja huku timu mbili ndizo zitakazo panda daraja baada ya kucheza 'play off' (mechi za mchujo) kwa timu mbili za juu katika msimamo wa ligi kwa kila kundi .

Makatibu hao wa klabu za ligi hiyo, walitoa ombi hilo katika kikao cha pamoja na viongozi wa Bodi ya Ligi Zanzibar sambamba na kamati ya kusimamia na kuendesha ligi kilichokuwa na lengo la kuangalia namna bora ya kuboresha ligi hiyo ya kanda msimu huu.

Kwa upande wa Katibu wa timu ya Raskazone, Mohammed Rashid 'Bwax', alisema bado bodi ya ligi wanayo muda wakukaa na kupeleka mapendekezo yao kwa kamati ya utendaji kuona wanapunguza idadi ya timu za kushuka daraja kutoka nane mpaka kuwa nne.

Alisema timu nane ni nyingi kushuka kwa pamoja kwa kuwa ligi hiyo inachezwa kwa makundi na klabu nyingi hazina fedha za uendesha hasa katika wakati huu wa ligi, hivyo bodi ya ligi haina budi kuangalia na kuzingatia maoni ya viongozi wa klabu hizo.

"Tunaomba kama ikiwezekana basi msimu huu mshushe timu nne tu badala ya nane, yaani kila kundi zishuke timu mbili badala ya kila kundi kushusha timu nne, klabu zetu ni maskini, hatuna uwezo wa kuziendesha, hivyo kushusha timu nane nikama hatujatendewa haki," alisema.

Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Issa Kassim, alisema amepokea maoni yote yaliyotolewa katika kikao hicho, hivyo kwa yale yanayoihusu bodi, yatapatiwa ufumbuzi wa pamoja na mengine yatawasilishwa kwa kamati ya utendaji na kamati ya mashindano ambao ndio waandaji wa kanuni.

Aidha, alizitaka klabu hizo kuhakikisha wanazisoma kanuni za mashindano na kuzifuta ili kuondokana na mambo ya mazoea ambayo yanafanywa na baadhi yao.

"Kitu kikubwa kitakachotufanya kufanikiwa kuboresha ligi hii ni kuondokana na mazoea, turudi katika utaratibu tuliyojiwekea, tukifata kwa kufuata taratibu na kuacha njia za makato basi tutafanikiwa," alisema.

MAOKOTO...




Mkuu wa Idara ya Uhusiano na Mawasiliano SportPesa, Sabrina Msuya (kushoto), akiwa na Meneja Biashara tiGO Pesa, Fabian Felician, baada ya kuchezesha droo ya kuwapata washindi wa simu janja na milioni moja kwa wiki ya kwanza ya Promosheni ya Maokoto Deilee, ambapo mshindi mkubwa ataondoka na Sh. milioni 15 huku kila siku wakitoa Sh. 20,000 kwa washindi 10. **MPIGAPICHA WETU**

# TBS yaibamiza ARU Bonanza la Viwango

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limeanza vema mashindano ya Viwango Sports Bonanza 2023 kwa kuibamiza mabao 21 timu ya mpira wa mikono ya Chuo Kikuu cha Ardhi, ARU.

Kwenye bonanza hilo la wiki moja timu sita za mchezo wa mpira wa miguu na mpira wa netiboli zitachuana kwa wiki nzima ambapo washindi watapewa zawadi mbalimbali. Akizungumza katika uzinduzi wa bonanza hilo, Katibu wa Michezo wa TBS, Nyabuchweza Magongo, alisema mashindano hayo yatafanyika wiki nzima ili waweze kupate washiriki wengi.

Alisema pia wamezindua uwanja wao wa mpira wa netiboli ambao umejengwa na menejimenti ya shirika hilo kwa ajili ya timu yao ya wanawake kufanya mazoezi.

Magongo alisema uwanja huo ni wa kisasa na umekidhi vigezo vyote vya kitaifa na kimataifa na kwamba hata timu ngeni zinazoshiriki bonaza hilo zimeufurahia.

Alisema bonanza hilo litashirikisha michezo mingi ukiwamo mpira wa miguu, netiboli, kuvuta kamba, mpira wa wavu, karata, pool table, mchezo wa bao.

Mmoja wa wachezaji wa mpira wa netiboli wa TBS, Johari Hamza, aliushukuru uongozi wa shirika hilo kwa kukubali kutenga wiki hii kuwa ya bonanza kwani licha ya kuimarisha afya zao itaongeza ari ya kazi na mshikamano miongoni mwao.

Alisema michezo imekuwa ikisaidia kwa kiwango kikubwa kuimarisha afya za watumishi na kuongeza upendo na ushirikiano miongoni mwao.

"Tunaomba bonanza kama hili liwe linafanyika kila mwaka kwa sababu limewaleta watumishi wote pamoja na wamefurahia kukutana sehemu moja kwa ajili ya michezo," alisema

Aliwataka Watanzania kujenga utamaduni wa kushiriki michezo mbalimbali kama sehemu ya kujenga mshikamano na kuimarisha miili yao kwani michezo ni afya.

# Dabo abaini tatizo la kukosa mabao Azam FC

**Na Saada Akida**

LICHA ya kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Tanzania Prisons, Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, ameeleza kukerwa na wachezaji wake kwa kushindwa kutumia nafasi wanazozipata.

Azam FC juzi walivuna alama tatu zingine katika mchezo wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuibuka na ushundi wa mabao 3-1 dhidi ya Prisons, kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Baada ya kukamilika kwa dakika 90, Dabo alisema bado ana kazi kubwa kwenye safu yake ya ushambuliaji kuitengeneza iweze kutumia vema nafasi wanazotengeneza ili kupata idadi kubwa ya mabao.

Alisema hakufurahishwa na wachezaji wake kushindwa kutumia nafasi wanazotengeneza huku wakionekana kuridhika mapema baada ya kupata bao la kuongoza badala kupambana kutafuta ushindi mwingine.

"Tunapata matokeo mazuri, lakini sijaridhishwa na jinsi wachezaji wangu wanavyocheza hasa pale tunapoongoza, tunashindwa kutumia nafasi tunazotengeneza. Kazi kubwa nitaifanya kipindi hiki ligi ikiwa imesimama kuhakikisha tunarejea na kuwa vizuri," alisema Dabo.

Aliongeza kuwa mchezo ulikuwa wa ushindani mkubwa kwa Tanzania Prisons kucheza mpira mzuri kwa kutengeneza nafasi nao kushindwa kuzitumia, hivyo alilazimika kufanya mabadiliko kwa kumtoa Lusajo Mwaikenda na kumuingia Yannick Bangala.

"Tulilazimika kufanya mabadiliko hayo baada ya Lusajo kuumia na Yannick kuchukuwa nafasi yake, alicheza vizuri, ninaimani atakuwa vizuri na msaada mkubwa kwa timu baada ya kupata muunganiko," alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Prisons, Fred Minziro, alisema wamefanya makosa ambayo yalikuwa faida kwa Azam FC kuwaadhibu mabao 3-1.

Alisema mchezo ulikuwa wa ushindani mkubwa na kutumia ufundi na mbinu na hatimaye Azam FC walifanikiwa katika mipango yao ya kuondoka na alama tatu.

"Wachezaji wamepambana, tumetengeneza nafasi na kushindwa kuzitumia, sasa tunarudi uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu yetu, kuhusu washambuliaji wangu kuna wachezaji watatu wa kigeni bado tunakamilisha utaratibu wa vibali vyao nina uhakika mechi ijayo nitawatumia," alisema Minziro.

Alisema ligi imekuwa ya ushindani mkubwa kuliko msimu uliopita, hivyo anarejea uwanja wa mazoezi kufanyia kazi yale yaliyojitokeza katika mechi mbili walizocheza kwa sababu hawataki kuwa sehemu ya timu itakayocheza 'Play off' mwishoni mwa msimu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MO SALAH AKOMALIWA

KLABU ya Al-Ittihad iko tayari kujaribu uamuzi wa Liverpool wanaosisitiza kuwa fowadi wa Misri, Mohamed Salah, 31, hauzwi kwa kutoa ofa ya dau la dola milioni 162 ili kumnunua mchezaji huyo. ***(CBS Sports)***

### HOJBJERG AFIKIRIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, 28. ***(Telegraph)***

### HENRY KUMRITHI SHAW

KLABU ya Manchester United imeulizia kuhusu beki wa Brentford, Rico Henry, 26, wakati wakitafakari chaguo la kujaza nafasi ya beki wa kushoto wa England, Luke Shaw, 28. ***(Mail)***

### MAGUIRE ANUKIA KUBAKI

MANCHESTER United wanatazamiwa kukataa ofa kutoka West Ham kwa mlinzi wa England, Harry Maguire, 30, huku kocha Erik ten Hag akitaka kumbakisha mchezaji huyo kutokana na matatizo yanayoongezeka ya majeruhi katika klabu hiyo. ***(talkSPORT)***

### ROWE ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA wanafikiria kuchelewa kumnunua kiungo wa kati wa Arsenal na England, Emile Smith Rowe, 23, huku wachezaji wawili wa Barcelona - fowadi wa Hispania, Ferran Torres, 23, na winga wa Brazil Raphinha (26), pia wakizingatiwa na 'The Blues' hao. ***(Mail)***

### SPURS KUMUUZA JOHNSON

KLABU ya Tottenham Hotspur imefanya mazungumzo na Nottingham Forest kuhusu mkataba wa kumnunua mshambuliaji wao raia wa Wales, Brennan Johnson, 22, lakini ofa rasmi bado haijawasilishwa kwa mchezaji huyo. ***(Sky Sports)***

### CANCELO KWA MKOPO

BARCELONA inatarajia kukamilisha mkataba wa mkopo kwa beki wa pembeni wa Manchester City, Joao Cancelo, 29, katika siku zijazo. ***(ESPN)***

### NDIDI AKARIBIA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest inakaribia kumsajili kiungo wa kati wa Leicester City na Nigeria, Wilfred Ndidi, 26. ***(talkSPORT)***

### BAKAYOKO AWINDWA LIVER

LIVERPOOL inashinikiza kumsajili winga wa PSV Eindhoven raia wa Ubelgiji, Johan Bakayoko, 20, huku Everton, Burnley na Crystal Palace pia wakimtaka mchezaji huyo. ***(Football Insider)***

### VLACHODIMOS ATAKIWA

KLABU ya Nottingham Forest imewasilisha ofa ya karibu euro milioni tisa kwa mlinda mlango wa Benfica na Ugiriki, Odysseas Vlachodimos, 29. ***(Fabrizio Romano)***

### SPENCE AWANIWA LEEDS

KLABU ya Leeds United imemtafuta beki wa kulia wa Tottenham Hotspur chini ya umri wa miaka 21, Djed Spence mwenye miaka 23 kwa uhamisho wa mkopo wa msimu mzima. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA
MAGAZETI YA ULAYA




# VINICIUS JUNIOR KUKOSA MECHI 8 REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

MCHEZAJI Vinicius Junior anatazamiwa kukosa mechi nane za Real Madrid ikiwamo mchezo wao wa dabi dhidi ya Atletico Madrid, vyanzo vimeiambia ESPN, baada ya kupata jeraha la paja katika ushindi wa bao 1-0 wa LaLiga Ijumaa dhidi ya Celta Vigo.

**"Kutokana na vipimo vilivyofanywa kwa Vini, mchezaji huyo amegundulika kuwa na jeraha kwenye msuli wa kulia," ilisema taarifa ya Madrid Jumatatu.**

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Vinicius mwenye umri wa miaka 23, anaweza kuwa nje ya uwanja kwa wiki sita kwa jeraha hilo la misuli.

Hiyo inamfanya fowadi huyo kukosa mechi sita za LaLiga dhidi ya Getafe, Real Sociedad, Atletico, Las Palmas, Girona na Osasuna, pamoja na mechi mbili za kwanza za Madrid za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Vinicius pia atakosa mechi ya Brazil ya kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Bolivia na Peru zitakazopigwa Septemba, mwaka huu.

Fowadi huyo alibadilishwa dakika ya 18 huko Vigo baada ya kuhisi maumivu wakati akikimbilia mpira.

"Alitaka kuendelea. Haikuwa mbaya sana," alisema kocha Carlo Ancelotti baada ya mechi.

"Kisha alijaribu kukimbia na ikaonekana kaumia na tukamtoa. Nadhani atarejea baada ya mapumziko ya kimataifa. Ni ajabu, alianza vizuri, alionekana kutozuilika."

●●● Alijaribu kukimbia na ikaonekana kaumia na tukamtoa, nadhani atarejea baada ya...


Madrid waliingia msimu wa 2023-24 wakiwa na washambuliaji watatu pekee katika kikosi chao cha kwanza: Vinicius, Rodrygo na Joselu aliyesajiliwa majira ya joto.

Ancelotti amekuwa akitumia mfumo wa 4-4-2 badala ya mfumo wake wa kawaida wa 4-3-3, huku Vinicius na Rodrygo wakishirikiana kushambulia.

Mfungaji bora wa timu hiyo hadi sasa ni mchezaji mwingine mpya, Jude Bellingham, ambaye amefanya vema katika nafasi ya namba 10, akiwa amefunga mabao manne katika mechi tatu za ligi.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,148,6
MECHI KALI
CHELSEA
VERSUS
AFC WIMBLEDON
1 | 1.14
X | 6.86
2 | 15.44
tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Augustine Kilwepu - 0657 093 XXX
2. Alhaji Bendela - 0658 388 XXX
3. Hamisi Msosa - 0659 844 XXX
4. Ismail Mambwembwe - 0675 130 XXX
5. Fatuma Kuru - 0675 594 XXX
6. William Makungu - 0676 032 XXX
7. Henry Noah Henry - 0679 894 XXX
8. Elina Amasi - 0717 040 XXX
9. Hassan Bakari - 0719 012 XXX
10. Issa Ally - 0719 731 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAMA WA RAIS WA TFF YA HISPANIA AGOMA KULA



**MADRID,** Hispania

MAMA mzazi wa rais wa Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF), Luis Rubiales, amejifungia kanisani na kusema yuko kwenye mgomo wa kula akipinga namna mwanawe anavyoshinikizwa kujiuzulu, binamu wa Rubiales ameiambia ESPN.

Angeles Bejar alijifungia ndani ya kanisa la Divine Shepherdess katika mji wa nyumbani wa Rubiales wa Motril, Andalusia kuanzia Jumatatu.

Alisema ameamua kufanya mgomo huo kwa sababu ya mwanawe kushutumiwa kwa kosa ambalo halina ukweli wowote.

Rubiales amesimamishwa kwa muda wa siku 90 kujihusisha na masuala ya soka na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), Ijumaa wakati Baraza Kuu la Michezo la Hispania pia linataka kumwondoa madarakani, kutokana na kumbusu mdomoni mchezaji wa Timu ya Taifa ya Wanawake, Jenni Hermoso.

Rais huyo alifanya hivyo baada ya Hispania kushinda Kombe la Dunia la Wanawake kwenye fainali iliyopigwa nchini Australia dhidi ya England.

Rubiales amekataa kujiuzulu kutokana na suala hilo, akisisitiza kwamba busu hilo lilikuwa la ridhaa - dai lililokataliwa na mchezaji huyo - na kutishia hatua za kisheria dhidi ya Hermoso.

Waendesha mashtaka wa Hispania walisema wamefungua uchunguzi wa awali wa unyanyasaji wa kijinsia katika tukio hilo.

Bejar aliiambia EFE mgomo wake utaendelea "kwa muda usiojulikana, mchana na usiku".

## Barca kusajili nyota kabla ya dirisha kufungw



**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta anaamini klabu hiyo bado ina uwezo wa kifedha kukamilisha idadi ya uhamisho kabla ya dirisha kufungwa.

Masuala ya kifedha yanayojulikana yamekatiza biashara ya Barcelona ya uhamisho katika misimu ya hivi karibuni na klabu hiyo imekuwa ikilenga kupata mauzo ya wachezaji ili kukomboa mishahara na kutengeneza nafasi kwa dili zozote zinazowezekana.

Ilkay Gundogan na Inigo Martinez wamewasili kwa uhamisho wa bure msimu huu wa majira ya joto, huku Oriol Romeu akikamilisha uhamisho kutoka Girona kwa ada ya karibu euro milioni nne.

Beki wa pembeni wa Manchester City, Joao Cancelo, anakaribia kujiunga kwa mkopo katika mkataba ambao utajumuisha chaguo la kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu, lakini Laporta haamini kuwa Barcelona italazimika

kukomea hapo.

"Nadhani tutakuwa na l cha kutosha cha mshal kutekeleza shughuli," alis Laporta. "Na kutakuwa na di ya mmoja."

Miongoni mwa walen wa Barcelona mwisho wa sha ni fowadi wa Atletico drid, Joao Felix, ambaye b yuko kwenye hali ya kug kucheza kule kwenye diml Wanda Metropolitano ba ya kukiri hadharani nia y ya kujiunga na Barca ms huu wa majira ya joto.

S43,241/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 02/09/2023 | 19:30 | Brighton & Hove Albion vs Newcastle United | 2.50 | 3.55 | 2.50 |
| 02. 02/09/2023 | 19:45 | Go Ahead Eagles vs SC Heerenveen | 2.60 | 3.60 | 2.39 |
| 03. 02/09/2023 | 20:00 | Portimonense SC vs Estrela Amadora | 2.60 | 3.15 | 2.65 |
| 04. 02/09/2023 | 14:00 | Glasgow Rangers vs Celtic Glasgow | 2.36 | 3.45 | 2.75 |
| 05. 02/09/2023 | 14:30 | KAA Gent vs Club Brugge | 2.32 | 3.55 | 2.70 |
| 06. 03/09/2023 | 15:00 | FC Andorra vs Tenerife CD | 2.19 | 3.00 | 3.45 |
| 07. 03/09/2023 | 16:00 | Kalmar FF vs Mjallby AIF | 2.25 | 3.00 | 2.90 |
| 08. 03/09/2023 | 17:00 | Union Saint-Gilloise vs Royal Antwerp FC | 2.31 | 3.35 | 2.85 |
| 09. 03/09/2023 | 17:15 | RCD Mallorca vs Athletic Bilbao | 3.00 | 3.00 | 2.40 |
| 10. 03/09/2023 | 17:30 | GD Chaves vs Moreirense FC | 2.29 | 3.20 | 3.05 |
| 11. 03/09/2023 | 17:30 | Estoril Praia vs Boavista Porto | 2.38 | 3.20 | 2.90 |
| 12. 03/09/2023 | 17:30 | FC Basel 1893 vs FC Zurich | 2.55 | 3.35 | 2.33 |
| 13. 03/09/2023 | 18:00 | Stroemsgodset IF vs Stabaek IF | 2.15 | 3.35 | 2.80 |
| 14. 03/09/2023 | 18:30 | IFK Norrkoping FK vs Djurgardens IF | 2.65 | 3.30 | 2.29 |
| 15. 03/09/2023 | 18:30 | Union Berlin vs RB Leipzig | 3.10 | 3.25 | 2.24 |
| 16. 03/09/2023 | 19:30 | KRC Genk vs RSC Anderlecht | 1.95 | 3.65 | 3.40 |
| 17. 03/09/2023 | 20:15 | Royal Charleroi SC vs St. Truidense VV | 2.17 | 3.35 | 3.10 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 30/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3540 | Seongnam Ilhwa vs Gimpo Citizen | 2.32 | 3.02 | 2.87 |
| 13:30 | 4804 | Dalian Aerbing vs Tianjin Teda | 3.81 | 3.10 | 1.94 |
| 13:30 | 5888 | Cheongju FC vs Anyang | 3.43 | 3.23 | 1.97 |
| 14:00 | 2112 | Phnom Penh vs National Defense Ministry FC | 1.30 | 5.33 | 6.97 |
| 15:00 | 4687 | Hull City U23 vs Millwall U23 | 2.86 | 4.03 | 1.99 |
| 16:00 | 1374 | FC Muza vs Zanaco | 1.64 | 3.08 | 5.65 |
| 16:00 | 3534 | Prison Leopards vs Power Dynamos | 3.08 | 2.68 | 2.43 |
| 16:45 | 2065 | Metallurg Bekabad vs Sogdiyona Jizzax | 2.75 | 2.75 | 2.55 |
| 16:45 | 2193 | Navbahor Namangan vs Otmk Olmaliq | 1.68 | 3.26 | 4.82 |
| 17:00 | 2187 | Colon de Santa Fe Reserve vs Huracan Reserve | 2.33 | 3.05 | 2.75 |
| 17:00 | 2544 | CA River Plate (Arg) vs Velez Sarsfield Reserve | 2.85 | 3.25 | 2.18 |
| 17:00 | 3678 | FK Silas vs FK Vilnus Bfa | 3.20 | 3.50 | 1.92 |
| 17:15 | 4559 | Akhmat Grozny vs Kryliya Sovetov | 2.00 | 3.46 | 3.20 |
| 17:15 | 5464 | Sochi vs CSKA Moscow | 3.16 | 3.21 | 2.12 |
| 18:00 | 1146 | NK Ilirija vs Rudar Velenje | 1.76 | 3.65 | 3.65 |
| 18:00 | 1248 | FC Kolin vs FK Chlumec | 2.29 | 3.41 | 2.70 |
| 18:00 | 1365 | Jiskra Domazlice vs Pribram | 3.61 | 3.25 | 1.94 |
| 18:00 | 1599 | TJ Sokol Lanzhot vs Zlin | 16.28 | 8.96 | 1.08 |
| 18:00 | 1902 | TJ Unie Hlubina vs Slovacko | 21.36 | 11.19 | 1.04 |
| 18:00 | 2336 | Siarka Tarnobrzeg vs Sokol Sieniawa | 1.11 | 8.55 | 12.22 |
| 18:00 | 2863 | FK Transinvest vs FA Siauliai B | 1.21 | 5.63 | 9.65 |
| 18:00 | 3726 | NK Fuzinar Ravne vs Brinje Grosuplje | 3.50 | 3.40 | 1.86 |
| 18:00 | 4026 | Lahti vs Inter Turku | 2.98 | 3.29 | 2.12 |
| 18:00 | 5375 | Polokwane City vs Mamelodi Sundowns | 7.78 | 4.20 | 1.38 |
| 18:30 | 4543 | Sokol Brozany vs Teplice | 9.13 | 5.68 | 1.23 |
| 19:00 | 1671 | Zob Ahan vs Havadar | 2.08 | 2.70 | 3.75 |
| 19:30 | 3096 | Baltika Kaliningrad vs Zenit St Petersburg | 3.72 | 3.36 | 1.87 |
| 19:30 | 3774 | Rostov vs Lokomotiv Moscow | 2.44 | 3.36 | 2.54 |
| 19:30 | 5820 | Pogon Szczecin vs Slask Wroclaw | 1.57 | 3.73 | 4.84 |
| 20:00 | 5606 | Talleres vs Colon Santa Fe | 1.89 | 3.20 | 3.86 |
| 20:30 | 1265 | Hittarps IK vs Varbergs Gif FK | 2.90 | 4.07 | 1.96 |
| 20:30 | 1481 | Chippa Utd vs Bloemfontein Celtic | 2.31 | 2.99 | 3.10 |
| 20:30 | 2090 | Stellenbosch vs Kaizer Chiefs | 2.67 | 2.87 | 2.72 |
| 20:30 | 2421 | Richards Bay FC vs Sekhukhune United | 2.92 | 2.87 | 2.51 |
| 20:30 | 3948 | Moroka Swallows FC vs Cape Town Spurs | 1.79 | 3.23 | 4.52 |
| 21:00 | 1679 | Zeljeznicar vs FK Igman Konjic | 1.66 | 3.46 | 4.79 |
| 21:30 | 2042 | Sampdoria vs Venezia | 2.12 | 3.24 | 3.24 |
| 21:30 | 4476 | Bari vs Cittadella | 2.21 | 3.09 | 3.19 |
| 21:30 | 4741 | Catanzaro vs Spezia | 2.93 | 3.19 | 2.30 |
| 21:30 | 5245 | Ternana vs Cremonese | 3.13 | 3.13 | 2.22 |
| 21:45 | 1160 | Harrogate vs Blackburn | 4.58 | 3.98 | 1.62 |
| 21:45 | 1339 | Sheffield Utd vs Lincoln | 1.35 | 4.77 | 7.36 |
| 21:45 | 3136 | Chelsea vs AFC Wimbledon | 1.14 | 6.86 | 15.44 |
| 21:45 | 5966 | Nottingham vs Burnley | 2.28 | 3.33 | 2.89 |
| 22:00 | 2663 | PSV Eindhoven vs Rangers | 1.54 | 4.10 | 5.03 |
| 22:00 | 3035 | AEK Athens vs Royal Antwerp | 1.74 | 3.57 | 4.27 |
| 22:00 | 5140 | Copenhagen vs Rakow Czestochowa | 1.65 | 3.65 | 4.74 |
| 22:00 | 5995 | Doncaster vs Everton | 7.36 | 4.77 | 1.35 |
| 22:15 | 5650 | Argentinos Juniors vs San Martin SJ | 1.56 | 3.51 | 5.69 |
| 23:00 | 4285 | Fortaleza (COL) vs Leones FC | 1.54 | 3.81 | 5.28 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KITAYOSCE SASA KUIVAA SINGIDA FG IKIWA KAMILI

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kitayosce ambayo mechi iliyopita ya Ligi Kuu Tanzania Bara ilicheza kwa mara ya kwanza tena dakika 14 tu na wachezaji wanane, kesho inatarajia kuingia dimbani Uwanja wa Liti Singida, kukipiga dhidi ya Singida Fountain Gate ikiwa kamili baada ya kumaliza changamoto ya vibali kwa wachezaji wake.

Meneja wa klabu hiyo, Rashid Ally, amesema kwa sasa wamemaliza changamoto zote zilizosababisha mechi yao dhidi ya Azam FC iliyochezwa Agosti 16 katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam na kuchapwa mabao 4-0 kuvunjika dakika ya 14 baada ya kuumia kwa wachezaji wake wawili hali iliyomlazimu mwamuzi Omari Mdoe kumaliza mchezo huo.

"Tumeshapambana kukamilisha mambo, kwa sasa kila kitu kiko sawa na tuna leseni zote za wachezaji, hivyo mashabiki watarajie tutakuwa na wachezaji 11 pamoja na wa akiba, lakini pia soka safi," alisema meneja huyo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Pendo Lema, alisema wanakwenda kucheza mechi ngumu kwani Singida Fountain Gate ni timu nzuri, lakini wamejiandaa vema.

"Tunakwenda kupambana na Singida Fountain Gate, tunajua kwa sasa imekuwa timu kubwa, imesajili wachezaji wengi wazuri na wazoefu kutoka ndani na nje ya nchi, wana mwalimu mzoefu wa soka la Tanzania, Hans van Pluijm, lakini na sisi tumesajili vizuri tunakwenda kwenye mechi hii tukiwa na malengo ya ushindi tukiwa pia tunaendelea kusajili ili kukiongezea nguvu kikosi chetu," alisema Lema.

Kitayosce ambayo pia inajiita Tabora United, imefanya usajili mwingine kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili kesho, Agosti 31.

Wachezaji hao ni Daud Rashid kutoka Geita Gold, Mahmoud Amir kutoka Coastal Union, Omari Mponda straika wa zamani wa Ndanda FC, Kagera Sugar na Ihefu, Innocent Joseph mchezaji aliyewahi kuzichezea Klabu za Stand United, Gwambina na Namungo FC.




Robertinho Oliveira

# Phiri avunja ukimya sakata na Robertinho

INATOKA UKURASA 24

wasioitakia mema Simba," alisema Try Again.

Aidha, Try Again, alisema malengo yao makubwa ni kutwaa mataji yote ya ndani wanayoshiriki ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara, kuvuka robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kufanya vizuri katika michuano ya Super League ndiyo maana walifanya usajili mkubwa kwa malengo.

Simba tayari imefanikiwa kutwaa taji la Ngao ya Jamii kwa ushindi wa penalti 3-1 dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga, mchezo uliopigwa Agosti 13, mwaka huu, Mkwakwani jijini Tanga.

Try Again alisema: "Kama bodi, Simba tulikaa chini, tukaangalia malengo yetu ya mwaka huu kutwaa ubingwa na kuvuka robo fainali, tunafikaje huko. Lazima uwe na nyezo katika mpira maana yake ni wachezaji na benchi la ufundi.

"Tumesajili wachezaji wengi wenye ubora na hizi sio hasira ila tumesajili kwa ajili ya mahitaji ya timu yetu ili kufikia malengo hayo ambayo hata mashabiki na wapezi wa Simba wanayatarajia," alisema Try Again.

Kuhusu usajili wa kiungo Frabrice Ngoma, kuwa wamemsajili kwa kuwapora Yanga, Try Again alisema wana uwezo mkubwa wa kuweza kusajili mchezaji yeyote wanayemtaka ndani ya timu hiyo.

"Nashangazwa na kauli za kudai waliporwa kiungo wa timu hiyo Fabrice Ngoma jambo ambalo halina ukweli wowote, Simba inapotaka mchezaji yeyote haiwezi kumkosa. Hizi stori za kuwa tumemchukuwa uwanja wa ndege ni maneno tu, maana tulimaliza dili la Ngoma wiki moja kabla ya kutua hapa nchini, kumpata haikuwa ngumu kwa sababu ya uhusiano mzuri kati yetu na Al Hilal," alisema na kuongeza:

"Ngoma ni mchezaji bora kwa Afrika, tumeweza kumnunua licha ya kukutana na vita vikubwa kutoka klabu zingine na si yeye hata usajili wa Willy Essomba Onana ulikuwa na changamoto kubwa siku ambayo tumemsajili kuna klabu ya Kaskazini mwa Afrika ikamtumia ujumbe kwenye simu yake ya mkononi na kumsumbua meneja wake kuachana na ofa yetu na kupewa pesa mara tatu zaidi tutakayompa, ulikuwa ugomvi mkubwa ingawa tuliweza kumbakisha."

Michezo
Jumatano Agosti 30, 2023
Nipashe



Vinicius kukosa mechi 8 UKURASA 21

# Phiri avunja ukimya sakata na Robertinho

●●● Asema yupo sana Simba, 'Try Again' naye aeleza mazito, amtaja Ngoma, Onana...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kimya cha muda mrefu huku akihusishwa na kutaka kuondoka kwa madai hana furaha kutokana na kukosa nafasi ya kucheza mara kwa mara, mshambuliaji wa Simba, Moses Phiri, amevunja ukimya kwa kusema bado yupo sana kueleza sababu ya kocha kutompa muda mwingi wa kucheza.

**Mashabiki wa Simba walikuwa wakipaza sauti mitandaoni na katika baadhi ya mechi wakisikika wakilalamika kitendo cha straika huyo aliyemaliza msimu uliopita akiwa na mabao 10 kabla ya kuumia, kutopewa nafasi na Kocha Mkuu, Robertinho Oliveira, huku baadhi ya vyombo vya habari (si Nipashe), vikidai hana maelewano na viongozi jambo ambalo umetoa maagizo kwa kocha kutompa nafasi.**

Lakini straika huyo kipenzi cha mashabiki wa Simba, ameibuka na kusema hana tatizo lolote na kocha mkuu wa timu hiyo, Robertinho na kwamba kutopata nafasi ya kucheza kwake kumesababishwa na kukaa nje akiuguza majeraha kwa muda mrefu huku akisisitiza kuwa hafikirii kuondoka ndani ya timu hiyo kwa sasa.

Phiri alisema hakuna ukweli juu ya kutaka kuondoka ndani ya kikosi cha timu hiyo na kuweka wazi ataendelea kusalia ndani ya klabu hiyo na kwamba hana matatizo na Robertinho licha ya yeye kukosa nafasi ya kucheza kwa muda mrefu ndani ya timu hiyo.

"Bado nipo sana Simba, nina mkataba nao hakuna ukweli kuwa nataka kuondoka hapa, ninafuraha na timu yangu na nitaendelea kupigania klabu yangu kila mechi kuhakikisha tunapata kile wanachokitarajia."

"Nashindwa kupata nafasi ya kucheza kwa sababu ya kutoka katika majeraha ambayo yaliniweka nje kwa muda mrefu, napewa muda mdogo ili kuweza kurudi taratibu kuweza kupambana hakuna kitu kingine," alisema Phiri.

Aliwaahidi mashabiki kupambania Simba kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kufikia malengo yao ya kutwaa mataji likiwamo la Ligi Kuu, Kombe la FA na kuvuka robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Simba, Salim Abdallah 'Try Again', kuhusu sakata hilo la Phiri, naye alikanusha taarifa za mshambuliaji kutaka kuondoka kutokana na madai kwamba hana furaha ndani ya kikosi cha timu hiyo baada ya kutopata nafasi chini ya Robertinho.

Aliwataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kuachana na maneno yatakayowavuruga na kuwakosanisha na viongozi, wachezaji na benchi la ufundi.

"Phiri ni mchezaji halali wa Simba hakuna ukweli wowote kuhusu kutaka kuondoka, Wanasimba wanatakiwa kutulia kuwapa muda viongozi, benchi la ufundi na wachezaji ili kutengeneza timu kuwa imara.

Alisema kulingana na usajili waliofanya kwa wachezaji wengi wapya wanatakiwa kupata muda wa kuzoea mazingira na kuingia kwenye mfumo wa kocha Robertinho.

"Sasa tuna mashindano mengi mbele yetu, ikiwamo Super League ambayo Tanzania tutazindua mashindano hayo, tunatakiwa kupata sapoti kwa mashabiki wetu na kuachana na maneno ya watu

INAENDELEA UKURASA 23



Moses Phiri.

## Dabo abaini tatizo la mabao Azam FC

**Na Saada Akida**

LICHA ya kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Tanzania Prisons, Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, ameeleza kukerwa na wachezaji wake kwa kushindwa kutumia nafasi wanazozipata.



INAENDELEA UKURASA 20

## Mama wa rais TFF ya Hispania agoma kula

**MADRID,** Hispania

MAMA mzazi wa rais wa Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF), Luis Rubiales, amejifungia kanisani na kusema yuko kwenye mgomo wa kula akipinga namna mwanawe anavyoshinikizwa kujiuzulu, binamu wa...



INAENDELEA UKURASA 22

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >